98. Kanuni.
99. Marekebisho yanayofanywa na Waziri.

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI  
MASHARTI YA MPITO NA MASHARTI YANAYOENDELEA**

100. Masharti ya mpito na yaliyohifadhiwa.

**SEHEMU YA KUMI NA TATU MAREKEBISHO  
YATOKANAYO**

**MAJEDWALI**

---

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



NA.10 YA 2015

NAKUBALI,  
JAKAYA MRISHO KIKWETE*Rais*

11 Mei, 2015

**Sheria kwa ajili ya kuweka pamoja masharti kuhusu usimamizi wa kodi kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa kodi na utekelezaji wa sheria za kodi zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania; kuweka mfumo wa thamani ya fedha unaozingatia mabadiliko ya thamani ya fedha na kuweka masharti yanahusiana na hayo.**

**IMETUNGWA** na Bunge la Jamhuri ya Muungano.

SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na tarehe  
ya kuanza  
kutumika kwa  
Sheria

**1.-(1)** Sheria hii itaitwa Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 na itanza kutumika kwa tarehe ambayo Waziri, kwa Tangazo litakalochapishwa kwenye *Gazeti la Serikali*, atateua.

Matumizi	<p><b>2.</b> Sheria hii itatumika Tanzania Bara, na Tanzania Zanzibar kwa Sheria zinazohusu usimamizi wa kodi ambazo zinatumiwa kwa pande zote mbili za Muungano.</p>
Tafsiri	<p><b>3.</b>-(1) Masharti ya Sheria hii kwa utekelezaji bora wa madhumuni ya Sheria hii, itazihusu sheria zote za kodi.</p> <p>(2) Msamiati wowote ambao hautatafsiriwa katika Sheria hii, kwa kadri utakavyokuwa ulazima katika kutekeleza sheria hii, utakuwa na maana sawa na iliyotolewa katika Sheria husika.</p> <p>(3) Kakika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-</p> <p>“makadirio ya kodi yaliyorekebisha” maana yake ni nimakadirio ya kodi yaliyobainishwa kwenye kifungu cha 48;</p> <p>“makubaliano” maana yake ni kitendo, mkataba, makubaliano, mtiririko wa matukio, shughuli, ahadi, maelewano, muamala au shughuli inayomhusisha mtu zaidi ya mmoja,, inajumuisha sehemu ya makubaliano;</p> <p>“makadirio ya kodi” maana yake ni ukokotoaji wa kiasi cha kodi unaofanywa na Kamishna Mkuu chini ya sheria ya kodi au kwa mtu amefanya tathmini mwenyewe na inajumuisha masuala yaliyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria hii;</p>
Sura ya 399	<p>“Mamlaka” maana yake ni Mamlaka ya Mapato Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mapato Tanzania;</p>



- “afisa muidhiniwa” maana yake ni afisa wa Mamlaka anayeshughulikia masuala yanayohusu sheria za kodi na ambaye ameidhinishwa kwa maandishi kutekeleza majukumu maalum kuhusiana na sheria yoyote ya kodi;
- Sura ya 408 “Bodi” maana yake ni ni Bodi ya Rufaa za Kodi ya Mapato iliyoundwa chini ya Sheria ya Rufaa za Kodi ya Mapato;
- Sura 399 “Kamishna Mkuu” maana yake ni Kamishna Mkuu aliyeteuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Mapato;
- “mali inayomilikiwa na mlipakodi iliyowekwa dhamana” maana yake ni mali inayoshilikiwa na wakala wa ukusanyaji kodi kwa mdhamana chini ya kifungu cha 60 au mali iliyowekwa kwenye dhamana chini ya kifungu cha 61;
- “uamuzi wa kodi” maana yake ni uamuzi wa Kamishna Mkuu kuhusiana na masuala ya kodi yanayowasilishwa na kundi la watu walio na maslahi sawa;
- “gharama za tozo na mauzo” kuhusiana na mali, maana yake ni gharama aliyoingia au ataingia Kamishna Mkuu au wakala aliyeidhinishwa kuhusiana na-
- (a) Kubaini au kuwezesha kulipwa tozo kuhusiana na mali; au
  - (b) kutwaa, kushiklia na kuuza mali iliyo chini ya dhamana;
- Sheria Na.1  
ya mwaka  
2005 “sheria ya forodha” maana yake ni Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- “thamani ya fedha” maana yake ni thamani iliyotajwa na sheria kuhusiana na kodi kwa madhumuni ya kuhifadhi thamani ya fedha dhidi ya mabadiliko ya thamani;

- “nyaraka” maana yake ni fomu za maandishi au za kielektroniki ambayo inajumuisha maelezo, tathmini, kitabu, cheti, hati ya madai, taarifa, kumbukumbu, marejeo ya kodi, au uamuzi;
- “jalada” kuhusiana na nyaraka, inajumuisha maingizo au utolewaji wa nyaraka ya maandishi au nyaraka ya kielektroniki;
- “kanuni za kiuhasibu zinazokubalika kwa ujumla” maana yake ni misingi ya kiuhasibu iliyoidhinishwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi;
- “mdhamini” maana yake ni mtu ambaye anamruhusu Kamishna Mkuu kuitumia dhamana kwa ajili ya malipo ya kodi au kulipwa na mlipakodi mwingine;
- “meneja” kuhusiana na kampuni yoyote, maana yake ni-
- (a) mshauri, mkurugenzi, meneja, mjumbe, afisa, au mtu mwingine anayeshiriki peke yake au pamoja na watu wengine kufanya uamuzi katika ngazi ya watendeji wakuu kwa niaba ya kampuni;
  - (b) mbia au mdhamini;
  - (c) mtu ambaye anachukuliwa kama meneja wa kampuni kwenye sheria nyingine ya kodi; na
  - (d) mtu ambaye maamuzi na maelekezo yake yanaigusa kampuni hiyo;
- “Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha;
- “uamuzi pingamizi” maana yake ni uamuzi kuhusiana na uamuzi ulitolewachini ya kifungu cha 52;
- “sheria nyingine za kodi” maana yake ni sheria nyingine za kodi mbali na Sheria hii zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania;

“mmiliki wa mali” inajumuisha mtu aliyepewa leseni chini ya Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Bidhaa kuhusiana na umiliki wa mtambo, gari, mnyama au kitu kingine kinachotumika kwa ajili ya uzalishaji, uuzaji au usambazaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru au kitu kingine chochote kilicho kwenye eneo linalotumiwa na mtu huyo kwa madhumuni hayo;

“mmiliki wa mali” inajumuisha-

- (a) kuhusiana na eneo au sehemu, maana yake ni mmiliki, meneja au mtu mwingine yeyote aliye kwenye maeneo au sehemu; na
- (b) kuhusiana na mali yoyote, maana yake ni mtu ambaye mali imekamatwa au kuchukuliwa kutoka kwake;

“uamuzi kwa suala binafsi” maana yake ni uamuzi wa Kamishna Mkuu kuhusiana na masuala ya kodi yaliyowasilishwa;

“kuzuia” inajumuisha kizuizini, kufungia, kuwekea alama, kuweka lakiri, kukamata, kunyang’anya au kuweka chini ya ulinzi;

“makadirio binafsi ya kodi” maana yake ni makadirio ya kodi yanayofanywa chini ya sheria ya kodi na mtu aliye na wajibu wa kuwasilisha marejeo ya kodi;

“kiwango kilichowekwa kisheria” maana yake ni kiwango cha punguzo la bei kilichoamuliwa na Benki Kuu ya Tanzania;

“kodi” kwa madhumuni ya usimamizi chini ya sheria hii, na inajumuisha kodi, tozo, ushuru, forodha adhabu na riba inayotolewa chini ya sheria ya kodi;

“manufaa ya kodi” kuhusiana na mtu maana yake ni faida anayopata mtu kwa-

- (a) kukwepa, kupunguza au kuchelewesha malipo ya deni la kodi;
- (b) kuongeza cha madai ya mtu ya marejesho ya kodi;

Sura ya 399

Sheria Na. 1  
ya mwaka  
2005

- (c) kuepusha au kuzuia makusanyo ya kodi; na
- (d) kitendo kingine chochote ambacho kwa maoni ya Kamishna , kinaweza kusababisha punguzo kwenye deni la kodi linalodaiwa;
- “mdaiwa wa kodi” maana yake ni mtu ambaye anadaiwa kodi ya Serikali;
- “sheria ya kodi inajumuisha-
- (a) sheria iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, isipokuwa haitajumuisha Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (b) sheria nyingine yoyote inayoweka masharti kuhusiana na Mamlaka ya Kusimaamia Kodi;
- (c) mkataba wowote wakimataifa uliofikiwa kwa mujibu wa kifungu cha 7; na
- (d) kanuni nyingine zozote zilizotungwa kwa mujibu wa kifungu cha 7 au zilizotungwa chini ya sheria yoyote iliyotajwa kwenye aya ya (a) au (b);
- “marejeo ya kodi” maana yake ni marejeo ya kodi yaliyotajwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria hii;
- “afisa kodi” maana yake ni afisa wowote wa Mamlaka anayeshughulikia masuala ya kodi kuhusiana na sheria yoyote ya kodi;
- “mlipa kodi” ni mtu yeyote anayewajibika kulipa kodi;
- “pungufu ya kodi” maana yake ni kiwango cha malipo ya kodi ambacho, kwa maoni ya Kamishna Mkuu, yangesababisha maelezo yasiyo sahihi, kama yasingegundulika;
- “gari” inajumuisha aina yoyote ya chombo cha kusafirishia watu au bidhaa ardhini;
- “chombo” inajumuisha aina zote za vyombo vya majini vya usafiri wa watu na bidhaa;
- “wakala wa kodi ya zui” maana yake ni mtu anayewajibika kuzuia malipo ya kodi ;

Sura ya 332 “kodi ya zuio” maana yake ni kodi ya mapato ambayo inatakiwa kuzuiwa na wakala wa zuio la kodi kwa mujibu wa Divisheni ya II ya Sehemu ya VII ya Sheria ya Kodi ya Mapato.

Thamani ya fedha

4.-(1) Kiwango cha fedha kilichorejewa kwenye sheria husika ya kodi, kwa madhumuni ya kukuza usawa kwenye mfumo wa kodi na kuweka kinga dhidi ya athali za mfumuko wa bei, kitafafanuliwa kwa mujibu wa thamani halisi ya fedha.

(2) Mfumo wa thamani ya fedha utatumika kuhusiana na adhabu zilizoainishwa chini ya Sheria hii na sheria nyingine ya kodi.

(3) Thamani halisi ya fedha itakuwa kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria hii.

(4) Waziri anaweza, kwa amri itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali kufanya marekebisho kwenye thamani ya fedha ili kuainisha mabadiliko yaliyopo kwenye orodha ya bei za walaji.

#### SEHEMU YA PILI SHERIA ZA KODI NA TAFSIRI ZAKE

##### (a) Sheria za Kodi

Mamlaka ya Kamishna Mkuu na Maafisa wa kodi.

5.-(1) Mamlaka ya Kamishna Mkuu, pamoja na mamlaka aliyonayo chini ya Sheria hii, yatatekelezwa kuhusiana na sheria nyingine yoyote ya kodi.

(2) Afisa wa kodi, katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, anaweza-

(a) kufanya kazi katika utekelezaji wa sheria moja ya kodi au zaidi kwa wakati mmoja; na

(b) kukusanya taarifa kwa madhumuni ya sheria yoyote ya kodi katika utekelezaji bora wa majukumu yake chini ya sheria mahususi ya kodi.

Uhusiano na  
Sheria za  
ushuru wa  
forodha

**6.**-(1) Endapo sheria ya forodha inatumika katika utozaji wa kodi ya ongezeko la thamani au ushuru wa bidhaa kwa bidhaa kuhusiana na bidhaa zinazolingizwa nchini au bidhaa zinazo safirishwa nje ya nchi na kuhusiana na masuala mengine kuhusiana na hayo, Sehemu za Kwanza, Pili, Tatu, Nne na Tano za Sheria hii zitatumika.

(2) Kamishna Mkuu, kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha ( 3), na pale ambapo sheria ya kodi inaelezea kuhusu masharti fulani kuhusiana na usimamizi wa sheria za forodha, anaweza kutumia masharti ya sheria hii badala ya kutumia masharti ya sheria hiyo ya forodha.

(3) Kamishna Mkuu atatekeleza mamlaka yaliyotolewa katika kifungu kidogo cha (2) kwa namna isiyokinzana na sheria ya forodha.

(4) Masharti ya Sehemu ya Pili (b), Tatu na Saba ya Sheria hii, yatumika katika usimamizi wa sheri aya forodha, kwa kiasi kwamba yataendana na masharti ya sheria ya forodha.

Mikataba ya  
kimataifa

**7.**-(1) Masharti ya makubaliano ya kimataifa, ambayo Jamhuri ya Muungano ni mwanachama, kwa kiasi ambacho hayakinzani na masharti yoyote ya kodi, yatakuwa na nguvu zaidi ya masharti yaliyotolewa na sheria za kodi.

*(b) Tafsiri ya Sheria za Kodi*

Mifumo ya  
upatikanaji  
wa maslahi ya  
kodi ambayo  
hayajafikia  
wakati wa  
kulipwa

**8.**-(1) Bila ya kujali masharti yoyote yaliyotolewa na Sheria hii, iwapo Kamishna Mkuu anaridhika kuwa mfumo wowote, ulionauwezo wa kutoa manufaa ya kodi kwa mtu yeyote, imeridhiwa au unatekelezwa-

(a) kwa madhumuni pekee ya upatikanaji wa manufaa hayo kwa madhumuni pekee ya kibiashara; au

- (b) kwa njia au namna ambayo kwa kawaida isingetumika kwa shughuli halali za kibiashara au kwa njia au namna ya kutambua haki au wajibu ambao si kawaida kuwepo kwa watu wanaofanya shughuli wakiwa karibu,

Kamishna Mkuu anaweza kuamua kiwango kitakacholipwa kwa kila kodi inayotozwa na Sheria hii, kama kwamba mfumo huo haukufuatwa au kutekelezwa au kwa mazingira ya hali hiyo, anaona inafaa kwa ajili ya kuzuia au kupangwa kwa thamani ya maslahi ya kodi itarajiwe kupatikana kutokana na mfumo huo.

(2) Uamuzi uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) utachukuliwa kuwa ni tathmini ya kodi na masharti ya Sheria hii na masharti mengine ya sheria ya kodi kuhusiana na tathmini yatatumika ipasavyo.

(3) Katika kifungu hiki “madhumuni ya kibiashara inayoendeshwa kwa nia njema” haitajumuisha upatikanaji wa manufaa ya kodi.

Utoaji wa taarifa ya ufafanuzi wa kodi

**9.-**(1) Kamishna Mkuu, anaweza kutoa maelekezo ya utendaji kuhusiana na ufafanuzi wa kodi kwa lengo la kuhakikisha usimamizi wa sheria za kodi na kuweka muongozo kwa watu wanaathirika na sheria hizo.

(2) Taarifa kuhusiana na ufafanuzi wa kodi-

- (a) itatolewa kwa njia ya waraka;
- (b) itaeleza bayana kuwa yaraka hiyo ni taarifa ya ufafanuzi wa kodi;
- (c) itakuwa na namba na kichwa cha habari ambcho kupitia kwake itatambulika;
- (d) itaanza kutumika kuanzia tarehe iliyotajwa kwenye taarifa hiyo ya ufafanuzi wa kodi au kuanzia ya kutolewa kwake.

Kufutwa kwa taarifa ya ufafanuzi wa kodi

**10.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza kufuta maelekezo ya utendaji yenye ufafanuzi wa kodi au sehemu yake.

(2) Kutungwa kwa Sheria au maelekezo ya utendaji yenye ufafanuzi wa kodi ambayo yanatofautiana na maelekezo ya kiutendaji yaliyopo yatahesabika kuwa yanafuta maelekezo ya kiutendaji kwa kiwango cha kutofuatiana huko.

Uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika kuhusiana na mfumo au mazingira maalum

**11.**-(1) Kamishna Mkuu, kwa maombi yatakayo wasilishwa, anaweza kutoa uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mfumo au mazingira maalum au uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana ambao utaelezea msimamo wa matumizi ya sheria ya kodi kuhusiana na makubaliano yanayopendekezwa kufikiwa-

(a) iwapo ni uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mfumo au mazingira maalum; au

(b) iwapo ni uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana.

(2) Uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mfumo au mazingira maalum na uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana unaweza kuzingatia mazingira mbalimbali au sheria mbalimbali za kodi.

(3) Endapo Kamishna Mkuu anatoa uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini mfumo au mazingira maalum au uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana kuhusiana na maombi au mtu aliye katika kundi liliainishwa, uamuzi huo utamfunga Kamishna Mkuu.

(4) Uamuzi uliotolewa chini ya kifungu hiki kitakuwa na nguvu-



- 
- (a) iwapo kabla ya matumizi, mwombaji anawasilisha-
- (i) taarifa kamili na ya kweli kuhusiana na vipengele vyote vya makubaliano ambayo uamuzi huo unamhusu;
  - (ii) mwenendo wa makubaliano kuhusiana na mambo yote ya msingi yaliyoainishwa kwenye uamuzi;
- (b) kuanzia tarehe uliyotolewa kwa kipindi kilicho ainishwa kwenye uamuzi huo.
- (5) Uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mfumo au mazingira maalum au uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana hautamfunga Kamishna Mkuu kuhusiana na mtu yeyote mbali na mwombaji au watu walio kwenye kundi maalum.
- (6) Mtu hatapinga uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mfumo au mazingira maalum au uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana, isipokuwa kwa pingamizi kuhusiana na uamuzi wa kodi.
- (7) Kwa madhumuni ya kifungu hiki kundi la watu inajumuisha-
- (a) wanachama wa asasi/kampuni; na
  - (b) watu ambao, kwa maoni ya Kamishna Mkuu, wanaweza kutambulika katika matumizi ya masharti fulani ya sheria za kodi.

Kukataliwa  
kwa maombi  
ya uamuzi  
kuhusiana na  
namna  
ambavyo  
kodi  
itatumika  
chini mfumo  
au mazingira  
maalum

**12.-(1)** Kamishna Mkuu anaweza kukataa maombi ya uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mfumo au mazingira maalum au uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana iwapo-

(a) ni uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini mfumo au mazingira maalum-

(i) makubaliano yamezingatiwa kwenye uamuzi wa kodi; au

(ii) Kamishna Mkuu ametoa maoni kuhusu uchunguzi kuhusiana na masuala ya kikodi ya mwombaji ambayo yanajumuisha makubaliano au kabla ya kuwasilishwa kwa maombi, na anamtaarifu mwombaji kwa maandishi kuhusiana na kusudio hilo;

(b) Kamishna Mkuu ana maoni kuwa taarifa ya ufafanuzi wa kodi iliyopo inazingatia makubaliano;

(c) maombi hayana umuhimu au yanaubishani;

(d) makubaliano hayajatekelezwa na kuna sababu za msingi za kuamini kuwa hayatatekelezwa;

(e) maombi hayajatoa taarifa ya kumuwezesha Kamishna Mkuu kufanya uamuzi; au

(f) kwa maoni ya Kamishna Mkuu ingekuwa si ustaarabu kutekeleza maombi kwa kuzingatia rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya

uitekelezaji na mambo mengine ambayo Kamishna Mkuu anaweza kuona yanafaa.

(2) Endapo ambapo Kamishna Mkuu anakataa kutoa uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mfumo au mazingira maalum au uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana, atamtaarifu mwombaji kwa maandishi sababu za kukataliwa huko.

Utolewaji  
uamuzi  
kuhusiana na  
namna  
ambavyo  
kodi  
itatumika  
chini mfumo  
au mazingira  
maalum

**13.-(1)** Kamishna Mkuu anaweza kutoa-

(a) uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mfumo au mazingira maalum kwa mwombaji kupitia taarifa ya maandishi; au

(b) mazingira maamlum au uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana kwa mwombaji kupitia taarifa ya maandishi na kuweka uamuzi wazi kwa umma.

(2) Kamishna Mkuu, katika kutoa uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mfumo au mazingira maalum au uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana, anaweza kutilia kuzingatia tukio lolote litakalotokea siku za mbele au masuala mengine ambayo ataona yanapaswa kuzingatiwa.

(3) Uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mfumo au mazingira maalum au uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana-

- (a) utaainisha masuala yaliyotolewa uamuzi, itatambua sheria za kodi, vipindi na mazingira ambayo uamuzi utatumika na fikra zingine zozote au mtazamo mwingine ambao unaweza kuathiri uamuzi huo;
- (b) iwapo ni uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini mfumo au mazingira maalum, utamtambua mwombaji pamoja na kutaja Nambari yake ya Utambulisho ya Mlipakodi; na
- (c) iwapo ni uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana, uamuzi huo hautaweka wazi utambulisho wa-
  - (i) mwombaji, isipokuwa kama mwombaji ameridhia kwa maandishi; au
  - (ii) Nambari ya Utambulisho ya Mlipakodi, wajumbe wa kundi au mtu mwingine aliyetambuliwa au kurejewa kwenye uamuzi, isipokuwa kwamba mwombaji anaweza kuidhinisha kwa maandishi kuwa utambulisho wake uwekwe wazi.

Kufutwa kwa uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mazingira maalum

**14.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza, kwa taarifa ya maandishi, kufuta uamuzi kwa ujumla au sehemu yake kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mfumo au mazingira maalum au uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana, au sehemu yake.

(2) Endapo uamuzi utafutwa kwa ujumla au kwasehemu chini ya kifungu kidogo cha (1) Kamishna

Mkuu-

- (a) iwapo ni uamuzi kuhusiana na namna ambavyo kodi itatumika chini ya mfumo au mazingira, atampa mwombaji taarifa ya kufutwa uamuzi huo; na

iwapo ni uamuzi wa wazi kuhusiana na kundi maalum la watu walio na maslahi yanayofanana, atawapa waombaji taarifa ya kufutwa huko na taarifa hiyo itawekwa wazi kwa umma.

SEHEMU YA TATU  
MAMLAKA YA MAPATO, WALIPA KODI NA WATAALAM  
WAELEKEZI WA KODI

*(a) Mamlaka ya Mapato*

Usimamizi  
wa sheria za  
kodi  
Sura ya 399

**15.** Mamlaka ya Mapato itakuwa na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa sheria za kodi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Uidhinishaji  
wa maafisa  
waidhiniwa

**16.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza kukasimu madaraka yake kwa maafisa wa kodi chini ya kifungu cha 16 cha Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhusiana na utekelezaji wa sheria za kodi.

(2) Kamishna Mkuu hatakasimu madaraka yake yaliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa mtu yeyote aliyetajwa kwenye vifungu vya 18 na 19.

(3) Afisa wa kodi, kwenye mazingira fulani au iwapo afisa aliyeidhinishwa kutekeleza mamlaka hayo, anaweza kutekeleza mamlaka chini ya sheria ya kodi.

Sura ya 399

(4) Kamishna wa Mapato aliyeteuliwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na kupewa madaraka ya kusimamia sheria yoyote ya kodi, anaweza kutumia mamlaka hayo kwa-

- (a) kubadilisha adhabu kuwa ya papo kwa papo kwa makosa chini ya kifungu 92 pale ambapo mtu anakiri kosa;
- (b) kutoa msamaha wa adhabu na riba chini ya kifungu cha 70; au
- (c) kurejesha kodi kwa mujibu wa kifungu cha 73.

Utambulisho wa maafisa kodi au maafisa waidhiniwa

**17.-**(1) Mamlaka itatoa kadi ya utambulisho kwa kila afisa wa kodi au afisa aliyeidhinishwa kutekeleza majukumu chini ya Sheria hii.

(2) Kadi ya utambulisho itakuwa na nembo ya Mamlaka na picha yenye ukubwa wa stempu ya afisa wa kodi au afisa aliyeidhinishwa.

(3) Endapo ambapo afisa wa kodi au aliyeidhinishwa anatekeleza mamlaka au majukumu kwa madhumuni ya usimamizi wa sheria ya kodi, afisa huyo ata vaa na kuonesha kitambulisho chake pale atakapotakiwa kufanya hivyo na mwananchi wa kawaida.

(4) Endapo ambapo afisa au afisa aliyeidhinishwa atashindwa kuonyesha kitambulisho kama atakavyoombwa afisa huyo au afisa aliyeidhinishwa hatafanya kazi zozote chini ya sheria ya kodi na mtumishi wa umma yoyote anaweza kukataa kufanya kazi na afisa huyo.

Wataalam

**18.-** (1) Mamlaka inaweza kumtumia mtaalam kwa vigezo na masharti ambayo Kamishna Mkuu ataona inafaa, ili kuisaidia Mamlaka kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

(2) Kamishna Mkuu atamsimamia mtaalam huyo.

(3) Mtu aliye na sababu za msingi za kukataa kushirikiana na mtaalam moja kwa moja, anaweza kukataa kushirikiana na mshauri huyo, lakini hatamzuia kufanya kazi zake.

(4) Endapo mtaalam anashirikishwa na kujulikana kwamba kushirikishwa kwake inawezekana ikaleta mgongano wa maslahi, mamlaka yaweza kusitisha ushirikishwaji wa mtalaam huyo baada ya kugundua mgongano huo wa maslahi.

(5) Mtu ambaye ana sababu za msingi kuamini kuwa mtaalam aliyeshirikishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) ana mgongano wa kimaslahi, atawasilisha malalamiko yake kwa Kamishna Mkuu.

(6) Endapo ambapo malalamiko yamewasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (5), Kamishna Mkuu, ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kupokelewa kwa malalamiko, atatoa uamuzi kuhusiana na malalamiko hayo.

Msaada wa  
maafisa wa  
taasisi za  
umma

**19.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza kuomba afisa kutoka katika taasisi ya umma au kuilinda Mamlaka katika utekelezaji bora wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

(2) Kamishna Mkuu atawasimamia maafisa waliorejewa chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa kumsaidia katika utekelezaji wa majukumu yake.

Malipo kwa  
ajili ya  
kutekelezwa  
sheria za kodi

**20.**-(1) Mtu hatastahili isipokuwa kama imeelezwa ipasavyo katika sheria ya kodi, kupata malipo au kurejeshewa gharama kutoka kwa Mamlaka kwa utekelezaji wa masharti ya sheria za kodi.

(2) Kifungu kidogo cha (1) hakitatumika kwa malipo ya-

(a) afisa wa kodi;

(b) mtaalam au ofisa wa umma ambaye anaisaidia Mamlaka katika utekelezaji wa majukumu yake.

(3) Malipo kwa ajili ya watu waliorejewa katika kifungu kidogo cha (2) yataamuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Sura ya 399

Utunzaji siri

**21.**-(1) Mtu ambaye ameajiriwa au aliajiriwa au kushirikishwa na Mamlaka kutoa msaada kwa Mamlaka, atatumza taarifa na nyaraka zote alizozipata, kutokana na ajira yake, kushirikishwa au zilizomfikia kuhusiana na sheria yoyote ya kodi, kwa usiri.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu cha (1), mtu anaweza kutoa taarifa au nyaraka zilizorejewa katika kifungu kidogo cha (1) iwapo utoaji wa taarifa hiyo -

(a) unafanywa kwa mtu ambaye ni mwajiriwa au aliyeshirikishwa na Mamlaka na taarifa hiyo inahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa ajira au shughuli;

(b) ni kwa madhumuni ya utekelezaji wa sheria ya kodi;

(c) iliyo idhinishwa na Kamishna Mkuu; au

(d) inatolewa mbele ya mahakana au baraza.

(3) Mtu anaweza kutoa taarifa na nyaraka zilizorejewa katika kifungu kidogo cha (1) kwa-



- (a) Waziri;
  - (b) kwa mtu yeyote aliyekatika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwenye idara ya ukusanyaji wa mapato au idara ya takwimu ambayo kwake utoaji wa taarifa hizo ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa makujumu ya kazi ya mtu huyo.
  - (c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu yeyote aliyeidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iwapo utoaji wa taarifa hizo ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ya kiofisi; au
  - (d) mamlaka husika ya Serikali ya nchi nyingine ambayo Jamhuri ya Muungano imeingia katika makubaliano ya kimataifa, kwa kiwango kilichokubalika chini ya makubaliano hayo.
- (4) Kifungu hiki hakitatumika kwa taarifa iliyochapishwa na kutangazwa chini ya mkataba kifungu cha 97.
- (5) Kifungu hiki hakitazuia utolewaji wa taarifa kuhusiana na mlipakodi mahususi kwenda kwa mlipakodi anayehusika au idhini ya maandishi ya mlipa kodi au mtu mwingine.

*(b) Nambari ya Utambulisho ya Mlipakodi*

Maombi kwa  
ajili Nambari

**22.-(1)** Mtu anayetakiwa kulipa kodi kutokana na uendeshaji wa biashara au shughuli ya

ya  
Utambulisho  
ya Mlipakodi

uwekezaji,atafanya maombi kwa ajili ya kupatiwa Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi ndani ya siku kumi na tano kuanzia tarehe ya kuanza kuendesha biashara hiyo.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo (1), Kamishna Mkuu anaweza kumtaka mtu yeyote kuomba kupatiwa Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi ndani ya kipindi ambacho Kamisha Mkuu atakaamua.

(3) Mtu anayemiliki Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi hataomba kupatiwa Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi nyingine.

(4) Maombi ya kupatiwa Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi yata-

- (a) kuwa katika fomu maalum iliyoainishwa;
- (b) ambatana na ushahidi wa maandishi kuhusu utambulisho wa muombaji; na
- (c) wasilishwa katika namna iliyoainishwa.

Utolewaji wa  
Nambari ya  
Utambulisho

**23.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza, kwa madhumuni ya utambulisho na uhakiki, kwa upande wa maombi yaliyofanywa chini ya kifungu cha 22, atampatia mtu Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi.

(2) Nambari ya Utambulisho ya Mlipakodi haitahamishwa au kutumiwa na mtu mwingine.

(3) Mtu atamiliki Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi moja na atatumia Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi hiyo kwa madhumuni ya sheria zote za kodi.

(4) Kamishna hatatoa Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi kwa mtu isipokuwa kama ameridhika -

- (a) na utambulisho halisi wa muombaji;

(b) kwamba mwombaji huyo hana Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi.

(5) Endapo Kamishna Mkuu atakataa maombi kwa ajili ya kupatiwa Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi, atampa mwombaji taarifa ya kukataliwa huko ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kupokelewa kwa maombi.

Matumizi ya  
Nambari ya  
Mlipakodi

**24.**-(1) Mtu ambaye amepatiwa Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi na Mamlaka ataijumuisha nambari hiyo kwenye kila madai, taarifa, marejesho, maelezo au nyaraka nyingine zilizowasilishwa kwa Mamlaka au kutumika kwa madhumuni ya sheria ya kodi.

(2) Isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo na Kamishna Mkuu, taasisi iliyotajwa kwenye Jedwali la Tatu, wakati wa kuingia katika shughuli ya kibiashara na mtu yeyote kuhusiana na masuala yaliyoainishwa kwenye Jedwali, atamtaka mtu huyo kutoa Nambari yake ya Utambulisho wa Mlipakodi.

(3) Mtu anayekusudia kutekeleza mpango wowote uliofanyika chini ya kifungu kidogo cha (2), atawasilisha kwa taasisi hiyo hati ya Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi au nakala iliyothibitishwa kuwa nakala halisi ya Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi.

(4) Kamishna Mkuu anaweza kuitaka taasisi iliyotajwa kwenye Jedwali la Tatu kuwasilisha kwake taarifa ya maandishi kuhusiana na-

(a) thamani ya shughuli za biashara zilizoainishwa kwenye safu ya Pili ya Jedwali la Tatu inayoendeshwa na na taasisi

hiyo ndani ya kipindi kilichotajwa kwenye taarifa ya Kamishna Mkuu; na

(b) majina, anuani na Nambari ya Utambulisho wa mlipa kodi za watu ambao mipango hiyo itafanywa kuendesha biashara hiyo.

(5) Taasisi yoyote ambayo imetakiwa kutoa maelezo hayo taarifa chini ya kifungu kidogo cha (4), itatoa taarifa hiyo kwa Kamishna Mkuu ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kutolewa kwa taarifa hiyo.

(6) Taasisi au mtu anayeenda kinyume na kifungu hiki anafanya kosa.

Ufutaji,  
ubadilishaji  
na  
marekebisho  
ya Nambari  
ya  
Utambulisho  
wa Mlipakodi

**25.**-(1) Kamishna Mkuu atafuta Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi iwapo ataridhika kuwa-

(a) mwenye nambari ya utambulisho amefariki au iwapo ni kampuni, imefilisika;

(b) mtu aliyetajwa kwenye Nambari ya Utambulisho wa Mlipa kodi ni mtu hewa;

(c) utambulisho wa mtu anayemiliki cheti hicho ni tofuati na utambulisho wa mtu ambaye kwake cheti kilitolewa;

(d) mtu ambaye kwake Nambari ya Utambulisho wa Mlipa kodi imetolewa anamiliki nambari nyingine ya utambulisho wa mlipa kodi;

(e) kuna sababu za msingi zinazopelekea kuhalalisha kufutwa kwa Nambari ya Utambulisho wa Mlipa kodi.

(2) Mtu anayemiliki Nambari ya Utambulisho wa Mlipa kodi atamtaarifu Kamishna Mkuu kwa maandishi kuhusiana na mabadiliko yaliyofanyika kwenye cheti, ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kufanyika kwa

Nambari ya Utambulisho wa Mlipa kodi.

(3) Kamishna Mkuu anaweza, pasipo kufuta hati ya Nambari ya Utambulisho wa Mlipa kodi, kumpatia mtu huyo hati ya Nambari ya Utambulisho wa Mlipa kodi iliyorekebisha pale itakapohitaji.

Haki ya  
kupata taarifa

**26.** Mamlaka itampatia taarifa kwa kila mlipa kodi taarifa kuhusu nafasi ya mlipa kodi kwa mujibu wa masharti ya sheria husika ya kodi.

Haki ya  
kuwakilishwa

**27.**-(1) Mlipakodi-

(a) atakuwa na haki ya kuwakilishwa katika masuala ya kodi; na

(b) atamtaarifu Kamishna Mkuu, kwa maandishi, baada ya kumteua mwakilishi.

(2) Mamlaka haiwajibiki kuwasiliana na mlipa kodi kupitia kwa mwakilishi wa mlipa kodi.

*(c) Wataalam Waelekezi*

Usajili na  
usimamizi wa  
wataalam  
waelekezi

**28.** Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya usajili na kufuta usajili wa wataalam waelekezi wa kodi na uendeshaji wa shughuli zao.

SEHEMU YA NNE  
MAWASILIANO RASMI NA NYARAKA

Lugha rasmi

**29.**-(1) Lugha rasmi kwa madhumuni ya usimamizi wa kodi zitakuwa ni na Lugha za Kiswahili na Kiingereza.

(2) Endapo mawasiliano yoyote au nyaraka ambazo ni muhimu kwa mlipa kodi kuhusu matumizi ya sheria ya kodi, si lugha rasmi, Kamishna Mkuu anaweza kumtaka mlipakodi kuwasilisha tafsiri rasmi ya mawasiliano yoyote au nyaraka hizo kwa maandishi.

Fomu na  
taarifa

**30.** Kamishna Mkuu anaweza kuainisha fomu zitakazotumika chini ya sheria ya kodi na atasababisha fomu hizo kupatikana kwenye ofisi za umma za Mamlaka na katika maeneo mengine na sehemu au aina nyingine ya mawasiliano kwa kadri atakayo ataamua.

Nyaraka  
zilizoidhini-  
shwa na  
zilizo na  
dosari

**31.**-(1) Nyaraka iliyotolewa na Kamishna Mkuu chini ya sheria ya kodi itakuwa imethibitishwa iwapo jina na cheo cha Kamishna Mkuu au afisa aliyeidhinishwa wa mamlaka-

(a) iwapo ni nyaraka ya karatasi, iliyochapishwa, wa kuchapishwa, kusainiwa na kupigwa muhuri; au

(b) iwapo ni nyaraka ya kielektroniki, iliyoingizwa kwenye nyaraka kwa njia ya sainsi ya kielektroniki.

(2) Tamko lililotolewa na mtu chini ya sheria ya kodi litakuwa imethibitishwa ipasavyo iwapo litasainiwa kwa madhumuni hayo na mtu huyo.

(3) Nyaraka iliyotolewa chini ya sheria ya kodi haitakuwa batili au kuwa na dosari iwapo-

(a) kimsingi inaendana na sheria ya kodi; na

(b) mtu ambaye nyaraka imeelekezwa kwake au inamhusu ametajwa kwenye nyaraka hiyo kwa mujibu wa maelewano ya pamoja.

(4) Endapo nyaraka imetolewa na Kamishna Mkuu chini ya sheria ya kodi ina dosari ambayo haihusiani na mgogoro wa tafsiri ya sheria au maelezo kumhusu mtu mahsus, Kamishna Mkuu anaweza kurekebisha nyaraka hiyo kwa madhumuni ya kurekebisha dosari hiyo.

Nyaraka zilizokwenye mfumo wa karatasi zilizowasilishwa kwa Kamishna Mkuu

**32.**-(1) Nyaraka iliyo kwenye mfumo wa karatasi itachukuliwa kuwa imewasilishwa kwa Kamishna Mkuu chini ya sheria ya kodi iwapo-

- (a) imewasilishwa kwenye ofisi za Mamlaka;
- (b) imetumwa kwa njia ya posta kwenda kwenye ofisi za Mamlaka; au
- (c) imetumwa kwenye sehemu nyingine yoyote ambayo Kamishna Mkuu ataelekeza.

(2) Nyaraka iliyorejewa kwenye kifungu kidogo cha (1) itachukuliwa kuwa imepokelewa na Kamishna Mkuu-

- (a) iwapo imetumwa kwa njia ya nukushi au njia ya kielekroniki muda ambao ujumbe ulitumwa;
- (b) iwapo imepelekwa kwa kumkabidhi afisa wa Mamlaka au kuiacha katika sehemu, muda ambao afisa alikabidhiwa au ambao nyaraka iliachwa kwenye sehemu hiyo
- (c) iwapo imepelekwa kwa njia ya kusajiliwa ya posta, katika muda ambao nyaraka iliwasilishwa au muda ambao mtu anataarifiwa kuwa nyaraka inamsubiri mtu huyo;
- (d) iwapo imetumwa kwa njia kya posta katika anwuani iliyo nje ya Jamhuri ya Muungano, siku kumi baada ya kupelekwa posta;

- (e) imetumwa kwa ya posta kutoka kwenye anwani iliyo nje ya Jamhuri ya Muungano, katika muda ambao nyaraka ingewasilishwa kikawaida kwa kupitia njia hiyo ya posta.

Nyaraka za karatasi zinazotolewa na Kamishna Mkuu

**33.**-(1) Nyaraka ya karatasi itachukuliwa kuwa imewasilishwa kwa mtu na Kamishna Mkuu chini ya sheria ya kodi iwapo-

- (a) imekabidhiwa kwa mtu au iwapo ni asasi na meneja wa asasi hiyo; au
- (b) imeachwa katika au imepelekwa kwa njia ya posta katika eneo la kawaida au sehemu ya mwisho ya makazi inayojulikana, biashara, ofisini, anwani ya posta au anwani nyingine ya mtu huyo ikijumuisha:
- (i) iwapo nyaraka imetumwa kwa njia ya posta iliyosajiliwa na mtu huyo amepewa taarifa kuwa nyaraka hiyo inasubiri kuchukuliwa na mtu huyo; au
- (ii) anwani iliyotajwa kwenye hati ya nambari ya utambulisho wa mlipakodi huyo.

(2) Nyaraka itachukuliwa kuwa imepokelewa katika mazingira yafuatayo-

- (a) iwapo imepelekwa kwa kumkabidhi mtu au kwa kuiacha katika sehemu au eneo, katika muda wa kumkabidhi mtu huyo au muda ambao iliachwa kwenye sehemu au eneo hilo;



- (b) iwapo imepelekwa kwa njia ya kusajiliwa ya posta, katika muda ambao nyaraka iliwasilishwa au muda ambao mtu anatarifiwa kuwa nyaraka inamsubiri mtu huyo;
- (c) iwapo imetumwa kwa njia ya posta katika anwani iliyo nje ya Jamhuri ya Muungano, siku kumi baada ya kupelekwa posta.
- (d) Iwapo uimetumwa kwa njia nyingine ya posta kwenda kwenye anwani iliyo nje ya Jamhuri ya Muungano, katika muda ambao nyaraka iliwasilishwa kikawaida kwa kupitia njia hiyo nyingine ya posta.

Mfumo wa  
kutuma  
nyaraka wa  
kielektroniki

**34.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza kuanzisha na kuendesha mfumo wa kielektroniki wa uwasilishaji wa nyaraka.

(2) Nyaraka za kielektroniki itachukuliwa kuwa imewasilishwa na mtu na kupokelewa na Kamishna Mkuu chini ya sheria ya kodi iwapo nambari ya uidhinishwaji wa nyaraka hiyo imetolewa kwa kutumia nambari ya uidhinishwaji mtu huyo.

(3) Masharti ya kifungu kidogo cha (2) hayatumika kwa mtu ambaye amemthibitishia, kwa kiasi cha kumridhisha Kamishna Mkuu kuwa hakutuma nyaraka au nyaraka ilitumwa bila idhini yake.

(4) Nyaraka ya kielektroniki itachukuliwa kuwa imepelekwa mtu na Kamishna Mkuu chini ya sheria ya kodi wakati namba ya usajili ya nyaraka imetolewa na nyaraka hiyo inaweza kutumiwa kwa uthibitisho wa mtu huyo kwa kutumia nambari ya uthibitisho wa mtu huyo.

(5) Kamishna Mkuu anaweza kuidhinisha nyaraka iliyochapishwa kuchukuliwa kama nakala ya

nyaraka ya kielekitroniki iliyowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) au iliyowasilishwa hiki au iliyotolewa chini ya kifungu hiki.

(6) Mahakama au baraza litakubali nakala ya nyaraka iliyoidhinishwa chini ya kifungu kidogo cha (5) kuwa ushahidi wa mwisho wa yaliyomo kwenye nyaraka ya kiilektroniki, isipokuwa kama itathibitishwa vinginevyo.

SEHEMU YA TANO  
UTUNZAJI WA NYARAKA NA UTOAJI WA TAARIFA

*(a) Utunzaji wa Nyaraka*

Utunzaji wa  
nyaraka

**35.-(1)** Kila mtu anayetoza kodi au mtu anayewajibika kulipa kodi atatunza ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atatunza nyaraka katika mfumo wa karatasi au mfumo wa kielektroniki ambazo-

- (a) zinakuwa taarifa zitakazo tolewa au zitakazowasilishwa kwa Kamishna Mkuu chini ya Sheria ya kodi;
- (b) zitawezesha uamuzi sahihi wa kodi inayotakiwa kulipwa chini ya sheria yoyote ya kodi kutolewa; na
- (c) zitaainishwa na Kamishna Mkuu au na kanuni.

(2) Kila mtu anayetoza kodi au mtu anayewajibika kulipa kodi atawajibika kumbukumbu na mahesabu kwa kuzingatia misingi inayotambulika kiujumla kuhusaina na utunzaji wa mahesabu na matakwa ya sheria husika ya kodi.

(3) Nyaraka zilizorejewa katika vifungu vidogo vya (1) na (2) zitatunzwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe husika au kwa kipindi kirefu zaidi kitakachotajwa kwenye sheria ya kodi.

(4) Iwapo mtu-

(a) anaweka pingamizi au anakata rufaa, nyaraka zote muhimu kuhusiana na suala lililo kwenye mgogoro zitahifadhiwa mpaka pale suala hilo litaamuliwa na maamuzi kutekelezwa;

(b) anafanya maombi kwa Kamishna Mkuu, Nyaraka zote zinazohusika na maombi zitahifadhiwa hadi hapo maombi hayo yatakapoamuliwa;

(c) anafanya maombi kwa ajili ya marejesho ya kodi, nyaraka zote muhimu kwa ajili ya ukokotoaji wa marejesho hayo zitahifadhiwa hadi hapo marejesho yatakapokamilika; na

(d) amepokea taarifa ya uchunguzi au ya ukaguzi wa mahesabu ya Kamishna Mkuu, nyaraka zote zitakazohusika na uchunguzi huo zitahifadhiwa hadi hapo Kamishna Mkuu atakapomjulisha mtu huyo kwa maandishi kuwa uchunguzi husika umekamilika.

(5) Kamishna Mkuu anaweza, kwa taarifa ya maandishi-

(a) kumuondolea mtu wajibu wa kutunza nyaraka au kupunguza muda ambao nyaraka zinatakiwa kutunzwa; na

(b) kumtaka mtu kutunza nyaraka kama ilivyoainishwa kwenye taarifa.

Matumizi ya  
mashine za  
kodi za  
kielektroniki

**36.**-(1) Mtu ambaye anauza bidhaa, anatoa huduma au anaepokea malipo kuhusiana na bidhaa zilizo uzwa au huduma zilizotolewa atatoa stakabadhi au ankara kwa kutumia mashine ya kodi ya kielektroniki.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Kamishna Mkuu, anaweza kuchapisha kwenye *gazeti* linalouzwa maeneo mengi au kwa kutumia chombo cha habari, kutangaza orodha ya watu au kundi la watu wasiotakiwa kutumia mashine ya kielektroniki au kutumia stakabadhi ya kielektroniki au ankara.

(3) Mtu yeyote asiyehitajika kununua au kutumia mashine ya kodi ya kielektroniki atatoa stakabadhi ya kawaida.

(4) Mtu atakayetoa stakabadhi ya kawaida ataingiza au kusababisha kuingizwa taarifa zifuatazo-

- (a) tarehe ambayo malipo yalifanyika;
- (b) jina kamili na anuani ya mtu aliyeuza bidhaa au aliyetoa huduma;
- (c) maelezo kamili ya bidhaa zilizouzwa au huduma zilizotolewa na taarifa kuhusiana na ubora na thamani ya bidhaa au kiasi kilichotozwa kwa huduma zilizotolewa ;
- (d) jina kamili na anuani ya mtu ambaye ameuziwa bidhaa au ambaye amepewa huduma;
- (e) Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi na;
- (f) maelezo mengine yoyote ambayo Kamishna Mkuu anaweza kuainisha kwa kupitia tangazo.

*(b) Uwasilishaji wa Taarifa za Mara kwa Mara*

Marejesho ya  
kodi

**37.**–(1) Marejesho ya kodi yanayowasilishwa na mtu binafsi itaeleza kuwa marejesho yamekamilika na ni sahihi na yatasainiwa na mtu aliyeitengeneza.

(2) Marejesho ya kodi yatakayowasilishwa na asasi yatasainiwa na-

(a) iwapo ni marejesho ya kodi ya mapato, meneja wa kampuni pamoja na mkaguzi wa hesabu aliye katika utumishi wa umma aliyethibitishwa ambao watatoa tamko kuwa marejesho hayo yamekamilika na ni sahihi; na

(b) iwapo ni kuhusiana na kodi nyingi yoyote, meneja ambaye atatoa tamko kuwa marejesho hayo yamekamilika na ni sahihi.

(3) Iwapo-

(a) mtu anafilisika au kampuni inafungwa au inafilisika;

(b) Kamishna Kuu ana sababu za msingi za kuamini kuwa mtu huyo-

(i) anakaribia kuondoka nchini moja kwa moja;

(ii) anakusudia kuacha kuendesha shughuli ya kibiashara ndani ya Jamhuri ya Muungano; au

(iii) ametenda kosa chini ya sheria ya kodi; au

(c) mtu anashindwa kuweka kumbukumbu kama inavyotakiwa na Sheria hii,

Kamishna Mkuu anaweza kumtaka mtu huyo kuwasilisha marejesho ya kodi katika tarehe ya awali kabla ya tarehe ambayo alitakiwa kuwasilisha marejesho ya kodi.

(4) Masharti ya Kamishna Mkuu yatakuwa kwa maandishi na yatawasilishwa kwa mtu yakielezea kipindi au sehemu ya kipindi au jambo lingine linalohusiana na marejesho ya kodi pamoja na tarehe amabayo marejesho yaliwasilishwa.

Msaada  
katika  
maandalizi ya  
marejesho

**38.**-(1) Mtu ambaye anaandaa marejesho ya kodi au kiambatanisho cha marejesho ya kodi kwa niaba ya mtu mwingine, atasaini marejesho hayo au kiambatanisho akithibitisha kwamba-

- (a) amekagua nyaraka husika za huyo mtu mwingine aliyetajwa chini ya Sheria hii; na
- (b) kwa ufahamu wake, marejesho, au kiambatanisho chake vinaonyesha kuwa ni mtazamo sahihi wa mazingira sahihi na ya haki kwa namna yanavyohusika.

(2) Kifungu kidogo cha (1) hakitatumika kwa mwajiriwa wa mtu anayewajibika kuwasilisha marejesho.

(3) Iwapo mtu aliyeandaa marejesho ya kodi au kiambatanisho chake chini ya kifungu kidogo cha (1) hajaridhika na taarifa zilioko kwenye nyaraka husika na maandalizi ya marejesho au kiambatanisho chake, mtu huyo atawasilisha taarifa ya maandishi kwa mtu huyo mwingine itakayoelezea sababu za kutokuridhika kwake na atasaini marejesho hayo huku akiweka msisitizo kuwa saini hiyo ni kwa ajili ya maelezo hayo mengine.

Uongezaji  
kwa muda wa  
kuwasilisha  
marejesho ya  
kodi

**39.**-(1) Mtu anayewajibika kuwasilisha marejesho ya kodi kwa mujibu wa sheria ya kodi anaweza kumuomba Kamishna Mkuu nyongeza ya muda wa kuwasilisha marejesho hayo.

(2) Maombi yaliyowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) yatakuwa kwa maandishi na yatawasilishwa ndani ya siku kumi na tano kabla ya tarehe inayotakiwa kuwasilishwa kwa marejesho hayo.

(3) Baada ya kupokelewa kwa marejesho chini ya kifungu kidogo cha (1), Kamishna Mkuu-

(a) anaweza kuongeza muda ambao ndani yake marejesho yalitakiwa kuwasilishwa; na

(b) atatoa taarifa ya maandishi kwa mtu huyo kuhusiana na uamuzi wa maombi yake.

(4) Nyongeza ya muda wa kuwasilisha marejesho hautazidi siku thelathini kutokea tarehe ya kuwasilishwa kwa marejesho.

(5) Kukubaliwa kwa nyongeza ya muda chini ya kifungu hiki hakutabadilisha tarehe ya malipo ya kodi kama ilivyoainishwa chini ya sheria ya kodi ambayo chiniyake marejesho yamefanywa.

Kushindwa  
kuwasilisha  
marejesho  
ya kodi  
kwa muda

**40.**-(1) Endapo mtu atashindwa kuwasilisha marejesho ya kodi ndani ya muda uliowekwa kwenye sheria ya kodi au kama ambavyo unaweza kuongezwa chini ya kifungu cha 39, Kamishna Mkuu anaweza kutumia, mamlaka aliyopewa chini ya Sheria hii, kumtuea mtu mwingine kuandaa na kuwasilisha taarifa hiyo.

(2) Uwasilishaji wa marejesho utakaofanyika baada ya tarehe iliyotajwa au kwa namna nyingine mbalimbali, na namna iliyoainishwa kwenye sheria husika ya kodi, hautakuwa na nguvu.

(3) Kamishna Mkuu atafanya makadirio kuhusiana na wajibu wa kulipa kodi kama itakavyohitajika na sheria ya kodi, ikijumuisha kwa njia ya marekebisho na kwa madhumuni haya, anaweza kutumia taarifa yoyote iliyo katika umiliki wa Kamishna Mkuu, ikijumuisha taarifa yoyote iliyopatikana chini ya vifungu vidogo vya (1) au (2).

Marekebisho  
ya  
marejesho  
ya kodi na  
taarifa  
nyingine

**41.**-(1) Endapo Kamishna Mkuu haridhishwi na marejesho ya kodi iliyowasilishwa kwake chini ya sheria ya kodi, atatumia mamlaka stahili, ikijumuisha ni pamoja na mamlaka yaliyotolewa kwenye sehemu ndogo ya (c) ya Sehemu hii kwa ajili ya kupata taarifa ya ziada kadri itakavyo haitahijika kwa ajili ya kufanya makadirio.

(2) Marejesho ya kodi ya yaliyowasilishwa, hayatarebishwa au kubadilishwa isipokuwa kama ilivyoainishwa kwenye sheria husika ya kodi.

(3) Kamishna Mkuu anaweza, katika kufanya makadirio au makadirio iliyorekebisha kuhusiana na marekebisho, kuzingatia taarifa yoyote iliyopokelewa chini ya kifungu kidogo cha (3).

*(c) Upatikanaji wa Taarifa na Raslimali*

Upatikanaji  
wa taarifa na  
raslimali

**42.**-(1) Kamishna Mkuu, pasipo kutoa taarifa ya awali, atakuwa na uhuru wa kuingia kwenye jengo lolote, kupata nyaraka yoyote, kukagua bidhaa, chombo gari, ndege au raslimali nyingine yoyote-

(a) iwapo ni nyumba ya kuishi au iwapo nyaraka au raslimali ipo ndani ya nyumba ya kuishi-

(i) kati ya saa 3 asubuhi na saa 12 jioni;  
na

(ii) katika muda mwingine wowote  
kama utakavyoruhusiwa kwa amri  
ya mahakama; na



(b) katika hali nyingine yoyote, katika muda wowote ule.

(2) Mamlaka ya Kamishna Mkuu yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) yanaweza kukasimiwa kwa afisa wa kodi.

(3) Wakati wa kutekeleza mamlaka yake chini ya kifungu kidogo cha (1), Kamishna Mkuu au afisa wa kodi anaweza-

(a) kutengeneza dondoo au kutoa nakala ya nyaraka yoyote ambayo ameipata;

(b) kukamata nyaraka yoyote ambayo inaotoa ushahidi ambao -

(i) ambao unaweza kuwa ni wa msingi katika kuamua wajibu wa kikodi wa mtu yoyote; au

(ii) unahusu kosa lililotendwa chini ya sheria ya kodi;

(c) kukamata raslimali ambayo kuhusiana nayo amepewa nafasi ya kuipata, iliyo na au inayotunza nyaraka kwa namna yoyote ile;

(d) iwapo nyaraka haipatikani au nakala yake haijatolewa kufuatia maombi ya mtu aliye na mamlaka juu ya nyaraka hiyo, kukamata rasilmali ambayo inaweza kufikiwa chini ya kifungu kidogo cha (1) ambayo Kamishna Mkuu au afisa muidhiniwa ana sababu za msingi za kuamini kuwa inazo au inatunza nyaraka hiyo katika hali yoyote ile.

(e) kuchukua sampuli ya bidhaa; na

(f) kugesha, kutia nanga, kuhifadhi au kutunza, kwenye jengo lolote au sehemu yoyote, gari lolote, ndege, chombo au kifaa kingine chochote kinachotumiwa na Kamishna Mkuu au afisa wa kodi.

(4) Nyaraka yoyote, rasilimali au sampuli iliyokamatwa chini ya kifungu kidogo cha (3) itatolewa huku ikiambatana na orodha ya mali zilizokamatwa iliyosainiwa na Kamishna Mkuu au afisa wa kodi na inaweza-

- (a) iwapo ni nyaraka iliyokamatwa, iliyozuiwa kwa kipindi kinachohitajika kwa ajili ya kufanya uamuzi wa wajibu wa kodi wa mtu au kwa ajili ya mwenendo wowote chini ya sheria ya kodi;
- (b) iwapo ni rasilimali iliyokamatwa, kuzuia rasilimali hiyo kwa kipindi ambacho kinahitajika kwa ajili ya uapitanaji wa nyaraka hiyo; au
- (c) iwapo ni sampuli, kuzuia sampuli hiyo kuuzwa kwa namna ambayo itaelekezwa na Kamishna Mkuu.

(5) Afisa muidhiniwa anayetekeleza mamlaka yake chini ya kifungu hiki anaweza kusaidiwa na kuambatana na mwajiriwa yeyote wa Mamlaka, mtaalam aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 18 au afisa wa umma anayetakiwa kutoa msaada chini ya kifungu cha 19.

Haki na  
wajibu wa  
mmiliki

**43.**-(1) Mtu yeyote anayemiliki jengo, eneo, nyaraka, bidhaa, kifaa, chombo, ndege au rasilimali yoyote ambayo afisa muidhiniwa anahitaji au ameipata chini ya Sehemu hii, anaweza kumtaka afisa huyo wa kodi kumuonyesha idhini.

(2) Iwapo afisa wa kodi anashindwa kutekeleza masharti yanayorejewa kwenye kifungu kidogo cha (1), mtu anaweza kumnyima afisa huyo fursa ya kuingia au anaweza kumtaka afisa huyo kuondoka kwenye jengo au eneo, au arudishe nyaraka au raslimali ambayo afisa huyo ameipata kwa wakati huo.

(3) Mtu anayemiliki jengo, eneo, nyaraka, bidhaa, kifaa, chombo, gari, ndege au raslimali ambayo kwake mamlaka chini ya Sehemu hii yanahusika, atatoa vifaa stahili na msaada kwa ajili ya utekelezaji bora kwa mamlaka yaliyotolewa chini ya kifungu hiki. masharti ya kifungu kidogo cha (3), afisa kodi atatumia mamlaka yaliyotolewa kwake chini ya kifungu cha 63 na atafanya maombi ya kibali cha upekuzi chini ya kifungu ya kifungu cha 94.

(5) Mtu anayemiliki nyaraka au raslimali zilizozuiliwa kwa mujibu wa Sehemu hii kwa gharama zake anaweza kuzichunguza nyaraka hizo na kutoa nakala au sehemu ya nyaraka hizo wakati wa masaa ya kawaida ya kazi chini ya uangalizi wa Kamishna Mkuu kama atakavyoamua.

(6) Endapo katika utekelezaji mamlakia yake hini ya nyaraka, raslimali au sampuli imepotea au imeharibiwa, Kamishna Mkuu atamlipa mmiliki wa nyaraka, raslimali au sampuli fidia inayofaa.

Notisi ya  
kupata  
taarifa

**44.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza, wa kupitia notisi ya maandishi, kumtaka mtu, ambaye hatakiwi kulipa kodi-

(a) kutoa taarifa yoyote iliyotajwa kwenye notisi;

(b) kuhudhuria kwa muda na sehemu iliyotajwa kwenye notisi kwa madhumuni ya kuhojiwa na Kamishna Mkuu au afisa aliyeidhinishwa na Kamishna Mkuu; au

(c) kutoa nyaraka yoyote iliyo chini ya mamlaka yake wakati wa mahojiano.

(2) Mtu yeyote anayetakiwa kuhojiwa chini ya kifungu kidogo cha (1) (b) anastahili uwakilishi.

(3) Notisi iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) itawasilishwa kwa mkono kwa mtu ambaye imeelekezwa kwake au kwa kuiacha kwenye sehemu ya kawaida ya biashara au makazi ya mtu huyo au kwa namna nyingine yoyote kadri ambavyo Kamishna Mkuu ataamua.

Ukaguzi wa  
hesabu za  
kodi au  
uchunguzi

**45.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza kutumia mamlaka yaliyotolewa kwake chini ya Sheria hii kukagua au kuchunguza masuala ya kodi ya mlipa kodi.

(2) Kamishna Mkuu anaweza kumchagua mtu yeyote ili akaguliwe kwa kuzingatia-

(a) historia ya mtu juu ya utekelezaji au ukiukwaji wa sheria yoyote ya kodi;

(b) kiasi cha kodi kinachotakiwa kulipwa na mtu huyo;

(c) aina ya biashara au shughuli nyingine yoyote inayoendeshwa na mtu huyo; au

(d) jambo lingine lolote ambalo Kamishna Mkuu anaona linafaa ili kuhakikisha ukusanywaji wa kodi inayodaiwa.

(3) Endapo mtu husika amekaguliwa au anachunguzwa kwa kipindi fulani, ukaguzi huo au uchunguzi hautamzuia mtu huyo kukaguliwa au kuchunguzwa kwa kipindi kinachofuatia iwapo kuna sababu za msingi zinazopelekea kuhitaji kukaguliwa au kuchunguzwa kwa mtu huyo.

(4) Ukaguzi au uchunguzi wowote unaweza kuendeshwa kwa madhumini ya sheria ya kodi zaidi ya moja.

**SEHEMU YA SITA  
WAJIBU WA MSINGI WA KULIPA KODI**

Makadirio  
na makadirio  
binafsi

**46.**-(1) Makadirio ya kodi yatafanywa kwa kutumia utaratibu wa makadiro binafsi iwapo mtu anayewajibika kulipa kodi anatakiwa kuwasilisha marejesho ya kodi.

(2) Hakuna mtu, mbali na Kamishna Mkuu, atakaye fanya marekebisho kwenye taarifa yoyote ya makadirio.

Makadirio  
ya dharura

**47.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza kufanya makadirio ya dharura kuhusiana na kodi inayotakiwa kulipwa na mtu chini ya sheria husika ya kodi-

(a) iwapo mtu huyo anatakiwa kuwasilisha marejesho ya kodi, chini ya mazingira yaliyo ainishwa kwenye kifungu cha 40(3) au la; na

(b) katika hali nyingine yeyote, iwapo mtu huyo anashindwa kuwasilisha marejesho ya kodi kwa muda unaotakiwa.

(2) Kamishna Mkuu atatumia maamuzi bora yaliyotangulia na taarifa zilizopo katika kufanya makadirio ya dharura.

(3) Makadirio ya dharura yanaweza kuwa halali kwa kipindi au vipindi au kuhusiana na shughuli au suala la msingi ambalo Kamishna Mkuu anaweza kuainisha kwenye taarifa ya makadirio.

(4) Makadirio ya dharura, isipokuwa kama Kamishna Mkuu ataelekeza vinginevyo kwenye taarifa ya makadirio, hayatamuondolea mtu wajibu wa kuwasilisha marejesho ya kodi au taarifa ya shughuli inayotozwa kodi kama itakavyohitajika na sheria yoyote ya kodi.

(5) Uwasilishaji wa marejesho za kodi hautaathiri makadirio ya dharura.

na mtu kuhusu na kodi hiyo basi, kipindi chochote cha kodi kinachohusiana na makadirio ya dharura kitahesabiwa dhidi ya kodi kuhusu kulipwa kuhusiana na makadirio mtu binafsi.

(7) Makadirio ya dharura yatachukuliwa kuwa yamefanyika chini ya sheria ya kodi ambayo mtu anawajibika kwake au kuhusiana na suala lililofanyiwa makadirio.

Makadirio  
yaliyofanyiwa  
marekebisho

**48.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza kufanya marekebisho kwenye makadirio ili kuhakikisha kuwa mlipakodi anawajibika kulipa kiasi sahihi cha kodi katika mazingira ambayo makadirio yanahusika.

(2) Iwapo, kwa maoni ya Kamishna Mkuu, mlipa kodi anashindwa kulipa kodi yoyote anayotakiwa kulipa kutokana na-

(a) kushindwa kutunza vitabu vya mahesabu, kumbukumbu au nyaraka kama inavyotakiwa kuwasilishwa chini ya sheria ya kodi au kutokana na dosari iliyofanyika kwenye vitabu, kumbukumbu au nyaraka; au

(b) kushindwa kwake kufanya au kuchelewa kuwasilisha marejesho yanayotakiwa chini ya sheria ya kodi au dosari au kutokujitosheleza kwa ritani yoyote,

Kamishna Mkuu anaweza kufanya makadirio ya kodi yanayodaiwa na riba yoyote inayotakiwa kulipwa kuhusiana na kodi hiyo ambavyo vyote vitatakiwa kulipwa ndani ya mwezi mmoja kuanzia tarehe ya kufanyika kwa makadirio, isipokuwa kama kipindi cha mbeleni kinaruhusiwa na Kamishna Mkuu.

(3) Kamishna Mkuu atatumia uamuzi mzuri na taarifa zilizopo katika kufanya marekebisho kwenye makadirio.

(4) Mamlaka ya Kamishna Mkuu ya kufanya marekebisho kwenye makadirio yatakoma baada ya miaka mitano kuanzia-

- (a) iwapo ni makadirio binafsi, tarehe ya uwasilishaji wa marejesho iliyopelekea makadirio kufanyika;
- (b) iwapo ni makadirio mengine halisi, tarehe ambayo Kamishna Mkuu anatoa taarifa ya makadirio kwa mlipa kodi; na
- (c) iwapo ni makadirio yaliyorekebishwa, tarehe iliyorejewa kwenye aya ya (a) au (b) ya makadirio halisi ya tathmini iliyofanyiwa marekebisho.

(5) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (3), hakutakuwa na ukomo kwa Kamishna Mkuu kufanya marekebisho kwenye makadirio iwapo suala linahusu udanganyifu, uzembe wa maksudi au ukiukwaji wa hali ya juu na au kwa niaba ya mlipakodi.

Sura ya 408

(6) Kamishna Mkuu hatarekebisha makadirio ya kodi ambayo tayari imerekebishwa au kupunguzwa kupitia uamuzi Bodi au Baraza, chini ya Sheria ya Rufani za Mapato ya Kodi au amri iliyotolewa na mahakama yenye mamlaka kamili.

(7) Makadirio ya kodi yatapoteza nguvu kuhusiana na marekebisho yaliyofanywa.

(8) Makadirio ya kodi yatachukuliwa kuwa yamefanyika chini ya sheria ambayo inamuwajibisha mtu au suala linalofanyiwa makadirio.

(9) Katika kifungu hiki, “makadirio halisi” maana yake ni makadirio ambayo si makadirio yaliyorekebishwa.

Taarifa ya makadirio

**49.-**(1) Endapo Kamishna Mkuu anafanya marekebisho chini ya sheria ya kodi, Kamishna Mkuu atatoa taarifa ya maandishi kuhusu makadirio kwa mlipa kodi katika namna iliyoelezewa chini ya vifungu vya 33 na 34.

(2) Pamoja na jambo lingine lolote lililoainishwa katika sheria ya kodi inayohusika, taarifa ya makadirio itataja-

- (a) jina la mlipa kodi na Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi;
- (b) makadirio ya Kamishna Mkuu kuhusu na kodi inayotakiwa kulipwa kwa kipindi hicho, shughuli au suala ambalo kwake makadirio yanahusika na kiasi ambacho bado kinatakiwa kulipwa;



- (c) sababu za Kamishna Mkuu kufanya makadirio;
- (d) tarehe ambayo kodi husika inatakiwa kulipwa; na
- (e) muda, sehemu na namna ya kupinga makadirio.

**SEHEMU YA SABA**  
**UTATUZI WA MIGOGORO**

Uamuzi  
kuhusu kodi

**50.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza, kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2) kufanya uamuzi kuhusu kodi, ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho au uamuzi, kutokutenda jambo lolote ambalo liko chini ya uwezo wake, uamuzi, maelekezo, maoni, idhini, ridhaa au jambo lolote litakalo mridhisha Kamishna Mkuu chini ya sheria ya kodi ambayo yamuathiri mtu yeyote moja kwa moja.

(2) Makadirio au uamuzi uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) hautajumuisha-

- (a) muongozi wa kiutendaji au uamuzi au kutotoa, uamuzi, kukataa au kufutwa kwa mwongozo wa kiutendaji;
- (b) uamuzi au kutotenda jambo lolote ambako kunamuathiri mtu kwa nafasi ya afisa wa kodi au mwajiriwa au wakala wa Mamlaka; au
- (c) kubadilisha adhabu kwa mtu anayekiri kosa ili kumuwezesha kulipa faini chini ya sheria ya kodi.

(3) Uamuzi wa kodi uliotolewa chini ya kifungu hiki utachukuliwa kuwa umetolewa-

- (a) iwapo ni makadirio binafsi, kwa tarehe ambayo marejesho ya kodi iliyotakiwa;
- (b) iwapo ni makadirio mengine, pale ambapo taarifa ya makadirio itanatolewa kwa mlipakodi; na
- (c) iwapo ni uamuzi mwingine wowote kuhusiana na kodi-
  - (i) iwapo sheria ya kodi inataja muda ambao kwake Kamishna Mkuu anatakiwa kufanya uamuzi; au

- (ii) Kamishna Mkuu anatoa taarifa ya maandishi ya uamuzi kwa mtu anayehusika.

(4) Kwa madhumuni ya Sheria hii, taarifa au nyaraka zifuatazo zitachukuliwa kuwa ni ushahidi wa mwisho kuwa uamuzi wa kodi umetolewa na ushahidi huo ni sahihi-

- (a) iwapo ni kuhusiana na makadirio binafsi, marejesho ya kodi ambayo yanapelekea makadirio kufanyika au nyaraka iliyotolewa na Kamishna Mkuu inayodaiwa kuwa ni marejesho ya kodi;
- (b) iwapo ni kuhusu makadirio mengine, taarifa ya makadirio au nyaraka uliotolewa chini ya mkono wa Kamishna Mkuu unaodaiwa kuwa ni nakala ya taarifa; na
- (c) iwapo ni kuhusu uamuzi mwingine wowote wa kodi, taarifa ya maandishi iliyotolewa chini ya mkono wa Kamishna Mkuu au nyaraka iliyotolewa chini ya mkono wa Kamishna Mkuu inayodaiwa kuwa ni memoranda ya uamuzi.

Kupinga  
uamuzi wa  
kodi

**51.**-(1) Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa kodi uliotolewa na Kamishna Mkuu anaweza kutoa pingamizi dhidi ya uamuzi huo ndani ya siku thelathini toka tarehe uamuzi huo ulipowasilishwa kwake.

(2) Mtu ambaye anayo sababu za msingi kupelekea kuongezwa kwa muda wa kutoa pingamizi dhidi ya uamuzi wa kodi, anaweza kufanya maombi kwa ajili ya kuongezewa muda.

(3) Endapo Kamishna Mkuu anaridhika na sababu zilizotolewa kwenye maombi yaliyowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (2), ataridhia maombi ya kuongezwa muda na atatoa taarifa ya uamuzi huo kwa mwombaji.

(4) Pingamizi kuhusiana na uamuzi wa kodi litakuwa kwa maandishi na litaelezea sababu za kutolewa kwake.

(5) Pingamizi kuhusiana na uamuzi wa kodi halitapokelewa isipokuwa kama mlipakodi amelipa kiasi cha kodi ambacho hakibishaniwi au moja ya tatu ya kodi iliyokadiriwa, au chochote kilicho kikubwa zaidi.

(6) Endapo Kamishna Mkuu anaridhirika kuwa kuna sababu za msingi za kupunguza malipo au kufuta malipo hayo, anaweza ama kufuta kiasi kinachotakiwa kulipwa chini ya kifungu cha (5) au kukubali malipo yaliyo pungufu.

(7) Endapo mlipakodi anaweka pingamizi na anafanya malipo chini ya kifungu kidogo cha (5), wajibu wa kulipa makadirio ya kodi iliyosalia utasitishwa hadi hapo pingamizi limeamuliwa kikamilifu.

(8) Katika kifungu hiki, “kodi isiyobishaniwa” kuhusiana na makadirio ya kodi au uamuzi wowote wa kodi maana yake-

- (a) kiasi cha kodi ambacho kinatakiwa kutozwa iwapo makadirio au uamuzi wa kodi unarekebishwa kwa mujibu wa pingamizi; na
- (b) kodi yote au makadirio ya kodi kuhusiana na bidhaa zilizoingizwa nchi.

Uamuzi  
kuhusiana na  
pingamizi

**52.**-(1) Kamishna Mkuu, baada ya kupokea pingamizi kwa mujibu wa kifungu cha 51, anaweza kufanya uamuzi ili kuamua pingamizi hilo au kuitisha ushahidi au taarifa yoyote kadri itakavyo onekana inafaa kwa ajili ya kuamua pingamizi, na anaweza, kwa misingi hiyo-

- (a) kurekebisha makadirio ya kodi kwa mujibu wa pingamizi hiyo na ushahidi wa ziada ambao atakuwa ameupokea;
- (b) kukataa kufanya marekebisho kwenye makadirio ya kodi.

(2) Endapo Kamishna Mkuu atakubali kufanya marekebisho kwenye makadirio ya kodi kwa mujibu wa pingamizi lililotolewa, atatoa taarifa kuhusiana na makadirio ya kodi ya mwisho kwa mweka pingamizi.

(3) Endapo Kamishna Mkuu-

- (a) anakusudia kufanya marekebisho kwenye makadirio ya kodi kwa mujibu wa pingamizi lililotolewa au ushahidi wa ziada; au

(b) anaamua kukataa kufanya marekebisho, atampatia mweka pingamizi taarifa itakayo ainisha sababu la kusudio hilo au uamuzi.

(4) Mweka pingamizi, ndani ya siku thethalini baada ya kupokea taarifa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3), atawasilisha maelezo yake kwa maandishi kwa Kamishna Mkuu iwapo Kamishna Mkuu anakubaliana na uamuzi wa kufanya marekebisho kwenye makadirio ya kodi au la.

(5) Kamishna Mkuu, baada ya kupokea maelezo ya mweka pingamizi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4), anaweza-

- (a) kufanya uamuzi kuhusiana na pingamizi kwa kuzingatia marekebisho yaliyofanyika kwenye makadirio ya kodi na mawasilisho yaliyofanywa na mweka pingamizi; au
- (b) kufanya uamuzi kuhusiana na sehemu ya pingamizi kwa mujibu wa mawasilisho ya mweka pingamizi.

Rufaa dhidi ya  
maamuzi ya  
pingamizi  
Sura ya 408

Sheria Na.1  
ya mwaka  
2005

**53.-** (1) Mtu ambaye hajaridhika na maamuzi kuhusiana na pingamizi au uamuzi mwingine wowote au kutokutenda chochote kwa Kamishna Mkuu chini ya Sehemu hii, anaweza kukata rufaa kwenye Bodi kwa mujibu masharti ya Sheria ya Rufaa za Kodi.

(2) Kifungu kidogo cha (1) kitatumika pia kwenye uamuzi au kutotoa uamuzi wowote chini ya sheria ya ushuru wa forodha.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Bodi itachukuliwa kuwa ni Baraza la Rufaa la Kodi lililoanzishwa chini ya kifungu cha 231 cha Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Afrika Mashariki.

## SEHEMU YA NANE

## MALIPO NA MAREJESHO YA KODI

*(a) Malipo ya Mara kwa Mara ya Kodi*

Muda wa  
kulipa kodi

**54.-** (1) Mlipa kodi atalipia kodi yoyote-

- (a) katika muda iliyotajwa kwenye sheria ya kodi ambayo chini yake kodi inatozwa;
- (b) iwapo kodi inayotakiwa kulipwa-
  - (i) kwa na makadirio ya dharura yaliyofanywa chini ya kifungu cha 47, katika tarehe iliyotajwa kwenye tangazo la makadirio lililotolewa chini ya kifungu cha 49; au
  - (ii) kwa makadirio yaliyofanywa chini ya kifungu cha 48, ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ambayo mtu aliyefanyiwa makadirio ya kodi anapelekewa taarifa kuhusiana na makadirio hayo chini ya kifungu cha 49;
- (c) iwapo ni kuhusiana na riba na adhabu iliyotolewa kwa mujibu wa Sehemu ya Kumi, tarehe iliyotajwa kwenye taarifa ya makadirio chini ya kifungu cha 81;
- (d) kuhusiana na kiasi kinachotakiwa kulipwa kwa Kamishna Mkuu chini ya kifungu cha 62(9), 68(2),69(2) au 62(5), kwa tarehe iliyotajwa kwenye tangazo;
- (e) kuhusiana na wajibu ulitolewa chini ya kifungu cha 65, katika muda ambao kodi ilitakiwa kulipwa na kampuni;

- (f) kuhusiana na kiasi anachotakiwa kulipwa Kamishna Mkuu chini ya kifungu 67(3) au (4), ndani ya siku saba baada ya kufanyika kwa mauzo ambayo kutoka kwake kiasi kinatengwa au kutotengwa, kama hali itakavyokuwa; au
- (g) kuhusiana na kiasi kinachotakiwa kulipwa kwa Kamishna Mkuu chini ya kifungu cha 68(5), kwa tarehe iliyotajwa kwenye karadha.

Uongezaji  
muda wa  
kulipa kodi

**55.-**(1) Mlipa kodi anaweza kumuomba Kamishna Mkuu kwa maandishi, kumuongezea muda wa kulipa kodi chini ya sheria ya kodi.

(2) Kamishna Mkuu, baada ya kupokea maombi na iwapo sababu za msingi zimetolewa, anaweza kusogeza mbele tarehe ambayo kodi au sehemu ya kodi ilitakiwa kulipwa

(3) Kamishna Mkuu atampa mwombaji taarifa kwa maandishi kuhusiana na maombi hayo.

(4) Endapo maombi ya kuongeza muda yanakubaliwa kwa kuruhusu mlipa kodi kufanya malipo kwa awamu na mlipa kodi anashindwa kulipa yoyote kati ya awamu zilizopangwa, kiasi chote kilichosalia pamoja na riba zitatakiwa kulipwa mara moja.

Namna na  
sehemu ya  
kulipia kodi

**56.-** (1) Mlipa kodi atalipa kodi-

- (a) kwenye ofisi yoyote ya malipo ya kodi;
- (b) katika benki iliyoidhinishwa kwa madhumuni hayo;
- (c) kwa kupitia mfumo wa malipo kwa njia ya simu za viganjani au mkononi; au
- (d) kwa namna nyingine itakayoainishwa na Kamishna Mkuu.

(2) Endapo mlipa kodi analipa kodi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), atamtaarifu afisa wa kodi wa sehemu ambayo mlipa kodi huyo amesajiliwa kuhusu malipo hayo.

(3) Mlipa kodi atalipa kodi kwa kupitia moja kati ya njia zifuatazo-

- (a) iwapo malipo yanafanywa kwenye ofisi ya kodi kwa fedha taslimu; au-
- (b) iwapo malipo yanafanywa kupitia benki kwa-
  - (i) fedha taslimu;
  - (ii) hundi;
  - (iii) kuhamisha moja kwa moja kwenye akaunti.

(4) Malipo ya kodi yatachukuliwa kuwa hayakufanyika iwapo hundi iliyowasilishwa kwenye benki imekataliwa.



Namna ya  
kulipa kodi

**57.** Endapo mlipa kodi analipa kodi chini ya sheria moja ya kodi au zaidi na anafanya malipo kwa kiasi kisichozidi kiwango kinachotakiwa kulipwa, Kamishna Mkuu, bila kujali mfumo ulioanzishwa chini ya kifungu cha 58, anaweza kuamua kiasi cha kodi kama ni kiasi ambacho kimeshalipwa.

Akaunti za  
malipo ya  
kodi za  
mlipakodi

**58.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza kuanzisha na kuendesha mfumo wa kieletroniki kuhusiana na akaunti za mlipakodi.

(2) Mfumo unaoweza kuanzishwa na kuendeshwa kipekee au kama sehemu ya mfumo wa kieletroniki wa mfumo wa nyaraka ulionzishwa chini ya kifungu cha 34.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wenye tija wa kifungu hiki, Kamishna Mkuu anaweza kutunga kanuni zinakazoainisha-

- (a) lini kodi itatakiwa kulipwa;
- (b) kodi iliyolipwa; na
- (c) mambo mengine yanayofanana na mambo yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 34.

*(b) Madai ya Kodi Kutoka kwa Mlipakodi*

Kesi  
kuhusiana na  
kodi ambayo  
haijalipwa

**59.**-(1) Endapo-

(a) malipo ya kodi yoyote hayajafika katika au kabla ya tarehe ambayo malipo hayo yanatakiwa kufanyika;

(b) taarifa iliyotolewa kwa mtu yeyote chini ya kifungu cha 81 haijatekelezwa,

kodi inayodaiwa inaweza kupatikana kwa njia ya deni la Serikali linaloweza kulipwa kupitia mashauri katika Mahakama yenye mamlaka stahiki.

Dhamana ya  
kodi (Karadha  
ya kodi) ya  
zuio

**60.**-(1) Kodi ya zuio ikijumuisha mali yoyote iliyopatikana kupitia wakala wa kodi ya zuio inaweza kupatikana kutoka katika mali au kiasi cha fedha-

(a) inayoshikiliwa kwa ajili ya dhamana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano;

(b) ambazo haziwezi kushikiliwa au kukamatwa kuhusiana na deni au wajibu wa wakala; na

(c) ambazo si sehemu ya mali inayotakiwa kufilisika au kufilisika kwa wakala.

(2) Kamishna Mkuu atakuwa na haki ya kwanza kudai malipo kuhusiana na kodi au mali kabla haijauzwa au kufuatia kufilisika kwa wakala wa kodi ya zuio.

Mauzo ya  
mali iliyo  
kamatwa

**61.**-(1) Endapo mlipa kodi anashindwa kulipa kodi kwa wakati unaotakiwa, Kamishna Mkuu anaweza kuweka tozo kwenye mali ya mlipakodi kwa ajili ya malipo ya deni la Serikali.

(2) Kamishna Mkuu atachukuliwa kuwa ameweka tozo iwapo anampelekea mlipa kodi taarifa ya

kodi ya zuio yenye kuainisha nambari ya mlipa kodi na Nambari ya Usajili wa Mlipa kodi, mali iliyokaguliwa, kiasi cha deni, kodi ambayo tozo inahusika na maelezo kuhusiana na mamlaka ya Kamishna Mkuu ya kuuza mali chini ya kifungu cha 62.

(3) Mali ya mlipa kodi itawekewa tozo kwa kuzingatia kiwango cha kodi ambacho hakijalipwa, riba inayotokana na kodi iliyotozwa chini ya kifungu cha 76 na gharama nyingine zozote kuhusiana na tozo na uuzaji.

(4) Tozo inayotozwa chini ya kifungu kidogo cha (2) haitakuwa na nguvu hadi hapo-

(a) iwapo riba katika ardhi au majengo iliyowekewa tozo, Kamishna Mkuu atakapowasilisha maombi kwa Msajili wa Hati chini ya kifungu cha (6) kuhusiana na tozo hiyo; na

(b) katika hali nyingine yoyote, taarifa inayohusu tozo itatumwa kwa mlipakodi.

(5) Tozo itaondolewa pale ambapo mlipa kodi atalipa kiasi chote kilichotajwa chini ya kifungu kidogo cha (3), kwa Kamishina Mkuu.

(6) Endapo Kamishna Mkuu ataweka tozo kuhusiana na ardhi au majengo, Msajili wa Hati atasajili tozo ya hati kuhusiana na ardhi au majengo bila malipo au ada yoyote.

(7) Endapo tozo kuhusiana na ardhi au majengo imetolewa, Msajili wa Hati ataondoa tozo usajili wa Hati kuhusiana na ardhi au majengo ndani ya siku thelathini na bila malipo au ada yoyote.

(8) Muamala wowote unaotekelezwa na Kamishna Mkuu chini ya kifungu hiki unaweza kupata msamaha wa ushuru wa stempu , na kodi nyingine yoyote ya muamala.

(9) Kamishna Mkuu anaweza kutoa taarifa ya maandishi kwa mlipa kodi-

- (a) itakayoeleza gharama za tozo kuhusiana na mali za mlipa kodi zilizolipwa na Kamishna Mkuu kabla ya tarehe ya kutolewa kwa taarifa; na
- (b) ikimtaka mlipa kodi kulipa gharama kwa Kamishna Mkuu ndani ya muda uliotajwa kwenye taarifa hiyo.

Mauzo ya  
mali  
iliyowekewa  
tozo

**62.**-(1) Kamishna Mkuu atampelekea mlipakodi taarifa ya maandishi kuhusiana na kusudio la kuuza mali zilizowekewa tozo zinazomilikiwa na mlipa kodi huyo.

(2) Taarifa iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) inaweza kuambatana na taarifa iliyotolewa chini ya kifungu cha 67 ikielezea:

- (a) jina la mlipa kodi na Namba yake ya Utambulisho wa Mlipa kodi;
- (b) mali aliyowekewa tozo, kusudio la Kamishna Mkuu la kuuza na njia inayopendekezwa na muda wa mauzo; na
- (c) iwapo ni mali isiyohamishika ambayo Kamishna Mkuu anakusudia kumiliki, namna na eneo ambalo umilikishwaji utafanyika.

(3) Katika utekelezaji wa mamlaka yake chini ya kifungu kidogo cha (1), Kamishna Mkuu-

- (a) anaweza kutekeleza mamlaka hayo ama moja kwa moja au kwa kupitia wakala aliyeidhinishwa;
- (b) atampatia mtu anayehusika nakala ya taarifa kabla ya kuchukua umiliki;
- (c) anaweza kuingia kwenye eneo au sehemu yoyote iliyotajwa kenye taarifa, kwa msaada wa polisi kwa madhumuni ya kulimiliki;
- (d) atampatia mlipa kodi orodha ya mali zilizokamatwa wakati atakapochukua umiliki; na
- (e) iwapo ni mali isiyohamishika , anaweza kuhifadhi mali, katika sehemu yoyote ambayo Kamishna Mkuu anaweza kuona inafaa, kwa gharama ya mlipa kodi.

(4) Kamishna Mkuu anaweza atauza mali iliyowekewa tozo baada ya kutoa taarifa kwa mlipakodi chini ya kifungu kidogo cha (1).

(5) Mauzo chini ya kifungu kidogo cha (4) hayatafanyika kabla ya-

- (a) iwapo ni mali au majengo, siku thelathini baada ya kuchukua umiliki;
- (b) iwapo ni mali zinayoweza kuharibika, siku moja baada ya kuchukua umiliki;
- (c) iwapo ni mali isiyohamishika, siku kumi baada ya kuchukua umiliki; na
- (d) iwapo ni kwa hali nyingine yoyote, siku kumi baada ya kuchukua umiliki.

(6) Mapato yatokanayo na mauzo yatumika kulipia-

- (a) gharama za kushikilia na kuuza mali; na
- (b) gharama za tozo na mauzo ya mali.
- (c) Malipo mengine yoyote ya kodi ambayo hayajalipwa

(7) Kamishna Mkuu, baada ya kugawa mapato yatokanayo na mauzo chini ya kifungu kidogo cha (6), atampatia mlipakodi taarifa ya maandishi itakayoelezea namna ambavyo mapato yatokanayo na mauzo yalitumika.

(8) Endapo kuna salio la pesa baada ya kufanyika kwa malipo chini ya kifungu kidogo cha (6), salio hilo litalipwa kwa mlipakodi baada ya kuwasilisha maombi ndani ya miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya mauzo na iwapo maombi hayajafanyika, salio litalipwa kwa Serikali.

(9) Endapo mapato ya mauzo hayatoshelezi kulipia gharama zote za tozo au mauzo, kodi inayodaiwa na riba iliyopatikana kuhusiana na kodi, Kamishna Mkuu anaweza kukusanya upya salio ambalo linadaiwa chini ya Sehemu hii au sehemu ndogo ya (c).

(10) Kifungu hiki hakitatafsiriwa kwamba kinazuia utekelezaji wa haki yoyote ambayo Kamishna Mkuu anayo kuhusiana na karadha iliyotolewa chini ya kifungu cha 60 au 61.

(11) Shughuli zinazoendeshwa na Kamishna Mkuu chini ya kifungu hiki hazitanzwa ushuru wa stempu na miamala mingine kuhusiana na kodi.

Kumzuia mtu

**63.**-(1) Endapo mtu anashindwa kulipa kodi kwa wakati uliowekwa na upo uwezekano wa mtu huyo kutoroka kutoka katika Jamhuri ya Muungano, Kamishna Mkuu anaweza, kwa taarifa ya maandishi au kwa njia nyingine yoyote ya mawasiliano kwa Mkurugenzi wa Uhamiaji, atoe amri ya kumzuia mtu huyo asiondoke nchini.

(2) Baada ya kupokea taarifa ya maandishi, Mkurugenzi wa Uhamiaji atamzuia mtu huyo kuondoka kutoka katika Jamhuri ya Muungano kwa kipindi cha siku kumi na nne baada ya tarehe ya kupokelewa kwa taarifa.

(3) Kamishna Mkuu ataondoa taarifa iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), iwapo atalipa kodi au mtu anayedaiwa ataweka utaratibu wa kufanya malipo kwa namna itakayomridhisha Kamishna Mkuu.

(4) Mahakama Kuu inaweza kuongeza muda uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) kufuatia maombi yaliyowasilishwa na Kamishna Mkuu.

Kuzuia mali

**64.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza, kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2)-

- (a) kuzuia bidhaa, gari, chombo au mali nyingine yoyote;
- (b) kuzuia na kupekua eneo lolote, sehemu, gari, chombo au mali yoyote ambayo anaamini kuwa bidhaa, chombo au gari lipo;
- (c) kuweka alama, kufunga au kuzuia jengo lolote, chumba, sehemu, vifaa vya kukusanyia au sehemu yoyote ya mtambo uliokenye kiwanda chochote, kodi zinazotozwa ushuru au vifaa

vilivyo kwenye kiwanda; na

(d) kutumia nguvu ya kawaida kwa madhumuni ya utekelezaji wa masharti ya aya za (a) na (b).

(2) Mamlaka ya Kamishna Mkuu yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo (1) yatatekelezwa iwapo Kamishna Mkuu anaridhika kuwa-

(a) kodi ya ongezeko la thamani kuhusiana na usambazaji wa bidhaa au uingizaji wa bidhaa nchini;

(b) chombo kimebeba mafuta yoyote ambayo tozo ya mafuta haijalipwa;

(c) tozo ya matumizi ya barabara haijalipwa kwa ajili chombo cha moto cha nje ya nchi;

(d) ushuru wa uingizaji bidhaa nchini kwa kipindi cha muda mfupi au ushuru wa uhamishaji haujalipwa kuhusiana na magari; au

(e) masharti yoyote ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa yaliyokiukwa kuhusiana na bidhaa zinazotozwa ushuru.

(3) Kamishna Mkuu anaweza kutekeleza mamlaka yaliyotolewa kwake chini ya kifungu kidogo cha (1) sambamba na mamlaka mengine yaliyotolewa kwa Kamishna Mkuu chini ya Sheria hii.

(4) Endapo Kamishna Mkuu atazuia mali chini ya kifungu kidogo cha (1)-

(a) atatoa taarifa ya maandishi kwa mmiliki wa mali; au

(b) iwapo hakuna mmiliki, ataiacha taarifa kwenye eneo au sehemu ambapo uzuiaji wa mali utafanyika.



- (5) Taarifa ya Kamishna Mkuu-
- (a) itataja mali na kuorodhesha mali zilizozuiliwa;
  - (b) itaelezea mali zilizozuiliwa chini ya kufungu hiki na sababu ya kuzizuia;na
  - (c) itaweka masharti kuhusiana na kuachiliwa na masharti ya uuzaji wa mali yoyote iliyozuiliwa.

(6) Kamishna Mkuu anaweza kuzuia mali kwa kipindi kinachotosha kwa sababu ya dharura au marekebisho ya makadirio wakati wa utekelezaji wa mamlaka yaliyotolewa chini ya vifungu vya 66 na 67.

(7) Endapo hakuna mtu ambaye atamridhisha Kamishna Mkuu, chini ya kifungu kidogo cha (6), kuwa anamiliki mali chini ya kifungu kidogo cha (1)(a), Kamishna Mkuu anaweza kuichukulia mali hizo kuwa ni mali iliyowekewa tozo na ataziua kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 62.

*(c) Madai ya Kodi Toka kwa Mtu wa Tatu*

Wajibu wa meneja wa asasi

**65.**-(1) Endapo asasi itashindwa kulipa kodi katika muda unaotakiwa, Meneja au mtu ambaye alikuwa meneja wa asasi ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili kabla ya asasi kufanya kosa hilo ataunganishwa na asasi kwa kosa la kuto lipa kodi.

(2) Masharti ya kifunga kidogo cha (1) hayatatumika pale ambapo meneja ametekeleza wajibu wake kwa uangalifu, uhakika na kwa maarifa ili kuzuia kosa la kushindwa kulipa kodi.

(3) Endapo mtu amelipa kodi chini ya kifungu kidogo cha (1) -

- (a) mtu huyo atarudishiwa malipo na asasi hiyo;

- (b) kwa madhumuni ya aya (a) mtu anaweza kuzuia mali yoyote ya asasi baada ya kuimiliki kwa kiasi kisichozidi malipo yanayotakiwa;
- (c) hakuna madai yanayoweza kufanyika dhidi ya mtu au asasi au mtu mwingine yeyote kutokana na salio lililobakizwa.

Mpokeaji wa mali

**66.**-(1) Mtu ambaye ameteuliwa kuwa mpokeaji wa mali atamtaarifu Kamishna Mkuu kwa maandishi kuhusu uteuzi wake, ndani ya siku kumi na nne tangu kuteuliwa kwake au kuhodhi mali zilizokuwa ndani ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Kamishna Mkuu anaweza kumpatia mpokeaji wa mali taarifa ya maandishi inayoonyesha kiasi ambacho kinaonyesha kuwa ni cha kutosha kutoa kodi yoyote inayotakiwa kulipwa au itatakiwa kulipwa na mlipa kodi ambaye mali zake ziko chini ya usimamizi wa mpokeaji wa mali.

(3) Baada ya kupokea taarifa chini ya kifungu kidogo cha (2), mpokeaji wa mali-

(a) atauza mali za kutosha ambazo zinahodhiwa na mpokeaji mali baada ya kutenga malipo ya madeni yote kwa kuzingatia kodi inayorejewa katika taarifa, kiasi kinachotolewa taarifa na Kamishna Mkuu chini ya kifungu hiki; na

(b) anawajibika kulipa kwa Kamishna Mkuu mahesabu ya kiasi ambacho kilitengwa kwa ajili ya kodi ya mlipa kodi.

(4) Mpokeaji wa mali kwa kiasi fulani, atakuwa ameshindwa kutenga kiasi kinachotakiwa na kifungu

kidogo cha (3), binafsi atawajibika kumlipa Kamishna Mkuu kwa ajili ya mlipa kodi wajibu wa kulipa kodi kwa kiasi ambacho kimewekwa lakini anaweza kurudishiwa kiasi chochote kilicholipwa kutoka kwa mlipa kodi.

(5) Kwa ajili ya kifungu hiki-

“mpokeaji” ina maana ya mtu yeyote ambaye kulingana na mali iliyoko ndani ya Jamhuri ya Muungano ni-

- (a) mfilisi wa asasi;
- (b) mpokeaji aliyeteuliwa nje ya mahakama au na mahakama kwa ajili ya mali au asasi;
- (c) mdhamini wa mtu aliyemfilisi;
- (d) mrehani;
- (e) msimamizi wa mali za marehemu;
- (f) uendeshaji wa mambo wa watu wasiojiweza.

Mdaiwa na  
mdhamini wa  
mlipakodi

**67.-(1)** Endapo mlipakodi atashindwa kulipa kodi kwa muda unaotakiwa, Kamishna Mkuu anaweza kutoa taarifa kwa maandishi kwa mtu mwingine anayedaiwa na huyo mlipakodi kulipa fedha kwa Kamishna Mkuu.

(2) Mtu mwingine anayedaiwa na mlipakodi akishapokea taarifa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), atalipa kwa Kamishna Mkuu kiasi cha fedha kinacholingana na jumla ya kodi inayodaiwa kwenye akaunti ya benki ya Kamishna Mkuu katika tarehe iliyoainishwa kwenye taarifa.

(3) Tarehe itakayoainishwa kwenye taarifa haitakuwa kabla ya-

- (a) tarehe ambayo fedha itapaswa kulipwa kwa mlipakodi au kuzuiliwa kwa niaba ya mlipakodi; au

(b) tarehe ambayo mtu mwingine anayedaiwa atapokea taarifa.

(4) Kamishna Mkuu atampatia mlipakodi nakala ya taarifa baada ya kuwasilisha taarifa kwa mtu mwingine anayedaiwa na mlipakodi.

(5) Kiasi kitakacholipwa kwa Kamishna Mkuu na mtu mwingine anayedaiwa na mlipakodi chini ya kifungu kidogo cha (2) au mdhamini kitahesabiwa kuwa ni kodi na italipwa ikiwa ni kodi.

(6) Zifuatazo zitachukuliwa kuwa ni fedha anayodaiwa mlipakodi-

(a) fedha ambayo inatakiwa kulipwa wakati huo au ambayo mlipakodi atatakiwa kulipwa baadae;

(b) fedha iliyozuiwa au ambayo baadae itatakiwa kuzuiwa kwa ajili au kwa sababu ya mlipakodi;

(c) fedha iliyozuiwa au ambayo baadae itatakiwa kuzuiwa katika akaunti ya mtu mwingine kwa ajili ya kulipwa kwa mlipakodi; na

(d) fedha iliyozuiwa na mtu ambaye ana madaraka aliyopewa na mtu mwingine ya kulipa fedha kwa mlipakodi.

Utekelezaji  
wa taarifa au  
karadha

**68.**-(1) Endapo mtu anayedaiwa kwa ajili ya mtu mwingine au mdhamini anayemlipa Kamishna Mkuu kwa mujibu wa kifungu cha 67 atachukuliwa kuwa amelipa kwa mamlaka ya mlipa kodi.

(2) Taarifa iliyotolewa chini ya kifungu cha 67 haitakuwa na nguvu iwapo kodi iliyotajwa italipwa au kufidiwa.

(3) Endapo mdaiwa wa pembeni ambaye amaepewa taarifa taarifa chini ya kifungu cha 67 atashindwa kutekeleza kutokana na ukosefu wa pesa kutokana na au inayoshikiliwa na mlipakodi, mdaiwa huyo kwa ajili ya mtu mwingine atamtaarifu Kamishna Mkuu kuhusiana na wajibu wake wa kulipa.

(4) Taarifa iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (3)-

(a) itakuwa ya maandishi na itaeleza sababu za kushindwa kutekeleza;

(b) itapelekwa kwa Kamishna Mkuu ndani ya siku saba baada ya kutolewa kwa taarifa chini ya kifungu cha 67 baada ya mtu anayedaiwa kwa ajili ya mtu mwingine kufahamau kuhusiana na utekelezaji wa taarifa kushindikana;

(5) Kamishna Mkuu, baada ya kupokea taarifa kutoka kwa mtu anayedaiwa kwa ajili ya mtu mwingine, anaweza kukubali au kuifuta au kuifanyia marekebisho taarifa iliyotolewa chini ya kifungu cha 67 au kuikataa taarifa ya mtu anayedaiwa kwa ajili ya mtu mwingine.

(6) Taarifa iliyotolewa na mtu anayedaiwa kwa ajili ya mtu mwingine chini ya kifungu hiki haitakuwa na nguvu isipokuwa kama Kamishna Mkuu anaifuta au kuirekebisha taarifa ya mtu anayedaiwa mtu anayedaiwa kwa ajili ya mtu mwingine iliyotolewa chini ya kifungu cha 67.

(7) Endapo mtu anayedaiwa kwa ajili ya mtu mwingine anashindwa kulipa kiasi cha kodi kilichotajwa kwenye taarifa ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya-

(a) taarifa kufikishwa kwake; au

(b) ambayo pesa ilimffikia au inataikwa kulipwa nayeye kwa mdaiwa, chochote kitakachotangulia na mlipa kodi-

(i) hajatoa taarifa chini ya kifungu kidogo cha (3) au kifungu hiki; au

(ii) ametoa taarifa ambayo imekataliwa na Kamishna Mkuu,

masharti ya Sheria hii kuhusiana na ulipwaji wa kodi yatatumika kuhusiana na ukusanyaji na ulipwaji kwa kiasi hicho, kama kwamba ilikuwa ni kodi iliyokuwa inatakiwa kulipwa na mtu anayedaiwa kwa ajili ya mtu mwingine, mtu anayedaiwa kwa ajili ya mtu mwingine tarehe iliyotajwa kwa ajili ya ulipwaji ambayo ndiyo ilikuwa ni tarehe ambayo kiasi kilitakiwa kulipwa kwa Kamishna Mkuu chini ya kifungu hiki.

Wakala watu wasio wakazi

**69.-(1) Endapo-**

(a) mlipakodi ambaye si mkazi atashindwa kulipa kodi kwa muda unaotakiwa; na

(b) Kamishna Mkuu anaamini kuwa mlipa kodi asiye mkazi hajalipa kodi ndani ya muda uliotakiwa,

anaweza, kwa taarifa ya maandishi, kumtaka wakala wa mtu ambaye anayeshikilia mali inayomilikiwa na mlipa kodi asiye mkazi ili kulipa kodi kwa niaba ya mlipa kodi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), wakala atatakiwa kulipa kodi kwa kiwango cha thamani ya soko ya mali kwa kiasi kisichozodi kiasi cha kodi ambacho mlipakodi anadaiwa.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki-

(a) mlipa kodi anayekodisha ndege au meli kwa

muda unaozidi miaka mitatu atachukuliwa kuwa anamiliki ndege au meli hicho cha majini katika kipindi hicho; na

(b) rubani wa ndege au nahodha wa meli atachukuliwa kwa wakati huo kuwa anamiliki ndege au meli hiyo.

(4) Kamishna Mkuu anaweza, kwa taarifa ya maandishi, kumtaka mbia mkazi kulipa kodi inayodaiwa au ambayo mbia mkazi anaweza kudaiwa.

(5) Mbia mkazi na mbia ambaye si mkazi watawajibika kwa pamoja au kila mmoja kulipa kodi kwa kiasi ambacho mchango wa mbia asiye mkazi anamiliki katika mali za ubia.

(6) Endapo malipo yatafanyika kwa Kamishna Mkuu kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) au (4)-

(a) mtu aliyefanya malipo anaweza kupata malipo kutoka kwa mlipa kodi au kwa mbia asiye mkazi;

(b) mtu aliyefanya malipo anaweza, kwa madhumuni ya aya ya (a), kubakiza kiasi cha mali yoyote ya mlipakodi au mbia asiye mkazi au aliye na umiliki au atamiliki kwa kiasi kisichozidi malipo yaliyofanyika; na

(c) mlipa kodi, mbia asiye mkazi au mtu mwingine yeyote hatamdai na mtu kuhusiana na kiasi kilichobakizwa.

#### SEHEMU YA TISA

#### MALIPO NA MAREJESHO YA KODI

Malipo

**70.** Endapo Kamishna Mkuu ameridhika kuwa kuna sababu za msingi za kuondoa adhabu au

riba zinazotowwa chini ya sheria yoyote ya kodi, anaweza kuondoa adhabu yote au sehemu ya adhabu au riba inayotakiwa kulipwa na mtu husika.

Maombi kwa  
ajili ya  
marejesho ya  
kodi

**71.**-(1) Mtu anaweza kumuomba Kamishna Mkuu marejesho kwa ajili ya malipo ya kodi yaliyozidi kodi inayotakiwa.

(2) Maombi ya marejesho ya kodi yatafanyika kwa maandishi, yakionyesha ukokotoaji sahihi wa kodi husika yakiambatana na ushahidi wa maandishi unaounga mkono maombi hayo.

Uamuzi  
kuhusiana na  
maombi

**72.**-(1) Kamishna Mkuu atafanyia kazi maombi na kutoa mamuzi kuhusiana na maombi yaliyowasilishwa chini ya kifungu cha 71 ndani ya siku tisini baada ya kupokelewa kwa maombi.

(2) Kamishna Mkuu, bila kuweka ukomo kwenye mamlaka yake, anaweza kufanya uamuzi unaofaa,-

- (a) iwapo ana maoni kuwa mwombaji hajalipa kodi ya ziada, wa kukataa maombi hayo;
- (b) iwapo hajaridhika kuwa mwombaji amelipa kodi ya ziada-
  - (i) kuomba taarifa ya ziada kama itakavyohitajika ili kumuwezesha kufanya uamuzi wa mwisho kuhusiana na maombi, au
  - (ii) kurejesha kodi ya ziada iliyolipwa kufuatia uwasilishaji wa maombi kwa ajili hiyo; au
- (c) iwapo anaridhika kuwa mwombaji amelipa kodi ya ziada kwa kiwango ambacho



Kamishna Mkuu ataridhika.

(3) Kamishna Mkuu atampatia mwombaji taarifa ya maandishi kuhusiana na uamuzi wa marejesho chini ya kifungu kidogo cha ( 1).

(4) Endapo Kamishna Mkuu anafanya uamuzi chini ya kifungu kidogo cha (2 ) (b) , Kamishna Mkuu atarejea upya uamuzi wake baada ya mwombaji kuwasilisha taarifa au iwapo mwombaji atakataa maamuzi hayo.

(5) Kamishna Mkuu atampatia mwombaji taarifa ya maandishi kuhusiana na uamuzi huo ndani ya siku thelathini baada ya kupokea taarifa iliyoombwa chini ya kifungu kidogo cha (2).

Malipo kwa  
marejesho ya  
kodi

**73.-**(1) Endapo, Kamishna Mkuu anaridhika kuwa mlipa kodi alilipa kodi ya ziada-

(a) atalipia ziada hiyo kwa lengo la kulipia kodi inayotakiwa kulipwa na mlipa kodi huyo chini ya sheria yoyote ya kodi; na

(b) atarudisha salio ndani ya siku kumi na nne kutokea kutolewa kwa uamuzi.

(2) Iwapo Kamishna Mkuu anakubali maombi ya mlipakodi kwa sehemu, atarudisha kiasi ambacho amekikubali.

(3) Endapo Kamishna Mkuu anarudisha kiasi cha kodi kwa mtu, atawajibika kumlipa mtu huyo riba kwa mujibu wa masharti ya sheria ya kodi inayohusika.

(4) Riba inayolipwa chini ya kifungu hiki itakokotolewa kwa kiwango kinachokubalika kisheria na itakuwa kwa kipindi kinachoanzia tarehe ambayo uamuzi wa marejesho unatolewa na kuishia siku

ambayo marejesho yalilipwa.

(5) Riba inayolipwa na mtu chini ya sheria ya kodi kuhusiana na kodi ambayo haijalipwa ndani ya muda uliotakiwa, kwa kiasi ambacho kodi itaonekana kuwa imelipwa, itarudishwa kwa mtu huyo pamoja na riba yoyote kwa kiwango kilichokokotolewa chini ya kifungu kidogo cha 4.

(6) Kamishna Mkuu atatumza akaunti tofauti ya benki na atahakikisha kuwa kuna fedha za kutosha kwa ajili ya madhumuni ya kifungu hiki.

Ushuru  
mdogo au  
uliolipwa  
kwake makosa

**74.** (1) Endapo ushuru wa forodha umetozwa kwa kiasi pungufu au umerudishwa kimakosa, mtu ambaye alitakiwa kulipa kiasi hicho likichopungua au ambaye marejesho yamelipwa kwake kimakosa, atalipa kiasi kilichotozwa au kulipa kiasi kilicholipwa kwake kimakosa.

(2) Kiasi kilichorudishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) kinaweza kulipwa kama kwamba kilikuwa ni kodi inayohusiana na kiasi kilichopungua au kilicholipwa kimakosa:

Isipokuwa kwamba, Kamishna Mkuu hatawasilisha madai baada ya miaka mitano kutokea tarehe ambayo kodi hiyo iliyopungua au malipo yaliyofanyika kwa kimakosa, isipokuwa kama kodi iliyopungua hilo au malipo yaliyofanyika kwa makosa yalitokana na udanganyifu wa mtu ambaye amelipa kodi iliyopungua au ambaye marejesho yalifanyika kwake kwa makosa.

SEHEMU YA KUMI  
RIBA, ADHABU NA MAKOSA

*(a) Riba*

Riba kwa  
makadirio  
madogo ya  
kodi  
inayotakiwa  
kulipwa

**75.**-(1) Kiasi cha riba ambacho mtu anayelipa kwa awamu anatakiwa kulipa chini ya kifungu kidogo (4), kitakokotolewa kwa mujibu wa sheria kwa kiwango cha kila mwezi, kiwango hicho kitatumika kwenye-

- (a) asilimia themanini ya kiasi chote cha kodi ambacho kingelipwa kwa awamu wakati wa mwaka huo wa mapato hadi mwanzoni mwa kipindi hicho iwapo makadirio ya mtu au makadirio yaliyofanyiwa mapitio yalikuwa sawa na kiasi stahili; au
- (b) kiasi cha kodi ya mapato kilicholipwa kwa awamu mwanzoni mwa kipindi cha mwaka wa mapato.

(2) Kwa madhumuni ya kukokotoa riba inayotakiwa kulipwa chini ya kifungu kidogo (1), muda wowote ulioongezwa chini ya kifungu cha 39 au 55 au usitishwaji uliotolewa chini ya kifungu 51(7) hautazingatiwa.

(3) Masharti ya kifungu hiki yatatumika pale ambapo malipo ya kodi ya mapato kwenye makadirio yaliyorekebishwa katika mwaka wa mapato kwa mujibu wa kifungu cha 85 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ni chini ya asiimia themanini ya kiasi sahihi.

Sura ya 332

Sura ya 332

(4) Endapo kifungu hiki kinatumika, mtu anayelipa kodi kwa awamu atawajibika kulipa riba kwa kila mwezi au sehemu ya mwezi kuanzia tarehe ya malipo ya awamu ya kwanza kwa mwaka huo wa mapato hadi kwa tarehe kodi inatakiwa kulipwa ambapo mtu atawasilisha marejesho ya mapato kwa mwaka huo wa mapato chini ya kifungu 91(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, “kiasi sahihi” maana yake ni kodi ya mapato inayotakiwa kulipwa na mlipakodi kwa mwaka huo wa mapato kwa mujibu wa kifungu cha 4(1)(a) na (b) cha Sheria ya Kodi ya Mapato.

Riba kwa  
kushindwa  
kulipa kodi

**76.-**(1) Endapo kiasi cha kodi iliyotozwa chini ya sheria ya kodi hailipwi baada ya tarehe iliyotajwa kwenye kanuni, kiwango cha riba kilichowekwa kisheria kitalipwa kwa Kamishna Mkuu kwa kipindi ambacho kilitakiwa kulipwa.

(2) Kwa madhumuni ya ukokotoaji wa riba inayotakiwa kulipwa chini ya kifungu kidogo (1), muda wowote ulioongezwa chini ya kifungu 39 au 55(1) au kusitishwa kulikofanyika chini ya kifungu 51(7) hakitazingatiwa.

(3) Wakala wa ukusanyaji wa kodi ya zuio anaweza kudai kutoka kwa mdaiwa kiasi cha riba kinacholipwa na wakala kuhusiana na kushindwa kutekeleza masharti ya kifungu cha 81, 82 au 83 cha Sheria ya Kodi ya Mapato.

*(b) Adhabu*

Adhabu kwa  
kushindwa  
kutunza  
kumbukumbu

**77.**-(1) Mtu aliyeshindwa kutunza kumbukumbu kama inavyohitajika kisheria atawajibika kutumikia adhabu kwa kila mwezi au sehemu ya mwezi

(2) Adhabu kwa mtu binafsi itakuwa ni pointi 1 ya thamani halisi ya fedha na iwapo ni kampuni itakuwa ni pointi 10 ya thamani halisi ya fedha.

(3) Kamishna Mkuu ataamua kodi itakayolipwa kwa kipindi kwa sababu halali na sababu ya msingi ikijumuisha kodi iliyotathminiwa kuhusiana na kipindi kirefu zaidi au kwa kutumia vipindi vya kodi vilivyojitokeza ndani ya kipindi hicho.

Adhabu kwa  
kushindwa  
kuwasilisha  
marejesho

**78.**-(1) Mtu anayeshindwa kuwasilisha marejesho ya kodi au kulipa kodi kwa muda uliotajwa na sheria ya kodi atawajibika kulipa adhabu kwa kila mwezi au sehemu ya mwezi kwa kipindi ambacho kutokutenda huko kunaendelea.

(2) Adhabu itakuwa-

(a) asilimia mbili nukta tano ya kiasi cha kodi kinachoweza kukadiriwa kuhusiana na marejesho ya kodi baada ya kupunguza kodi iliyolipwa mwanzoni mwa kipindi kuhusiana na kiasi hicho; au

(b) iwapo ni mtu binafsi, pointi 5 ya thamani halisi, au iwapo ni kampuni, pointi 15 ya thamani halisi, yoyote iliyo na thamani ya juu zaidi.

(3) Adhabu itatozwa kwa kila kosa la kushindwa kuwasilisha marejesho ambayo ni makadirio

au makadirio ya awali na kwa kushindwa kuwasilisha marejesho ya kodi iliyoambatana na makadirio ya mwisho.

Adhabu kwa kutoa taarifa ya uongo au ya kupotosha

**79.**-(1) Mtu atawajibika kulipa adhabu iwapo-

- (a) atatoa maelezo ya uongo au maelezo yanayopotosha kwa afisa wa kodi; au
- (b) hatatoa kwa afisa wa kodi maelezo ambayo, kwa kutotolewa kunasabisha upotoshaji katika maelezo hayo.

(2) Adhabu-

- (a) iwapo taarifa au kosa linafanyika bila ya sababu ya msingi itakuwa, asilimia hamsini ya kodi iliyopungua; au
- (b) iwapo taarifa au maelezo ya uongo yanatolewa kwa makusudi au kwa uzembe, itakuwa ni asilimia mia moja ya kodi iliyopungua.

(3) Bila kujali kifungu kidogo (2), adhabu;

- (a) itaongezwa kwa asilimia kumi kuhusiana na maombi yaliyotolewa kwa mara ya pili au yatakayofuatia italipwa na mtu huyo; na
- (b) itapunguzwa kwa asilimia kumi iwapo mtu anatoa taarifa kwa hiari yake kabla ya kugundulika kwake na afisa wa kodi au ukaguzi unafuatia wa mtu huyo.

(4) Taarifa itachukuliwa kuwa imetolewa kwa afisa wa kodi katika utekelezaji wa majukumu yayake chini ya sheria ya kodi iwapo imetolewa kwa maneno, kwa maandishi au namna nyingine yeyote na itajumuisha taarifa inayotolewa-

- (a) katika nyaraka yoyote au taarifa yoyote inayotakiwa kuwasilishwa kwa mujibu wa sheria ya kodi;
- (b) katika nyaraka iliyotolewa kwa afisa wa kodi mbalina nyaraka iliyotolewa chini ya sheria ya kodi; au
- (c) wakati wa kujibu swali lililoulizwa na mtu kwenda kwa afisa wa kodi;
- (d) kwa mtu aliye na ufahamu au matarajio ya msingi kuwa taarifa itatolewa kwa afisa wa kodi.

(5) Mtu anakayekiuka kifungu cha 23(3), 24(5) au 27(1)(b), atachukuliwa kuwa ametoa taarifa za uongo au zinazopotosha kwa afisa wa kodi.

Adhabu kwa kusaidia na kushinikiza

**80.** Mtu atakayemsaidia, kumshinikiza, kumshauri au kushawishi mtu mwingine kutenda kosa akipatikana na hatia atawajibika kulipa adhabu ya asilimia 100 ya kodi iliyopungua.

*(c) Makadirio ya Riba na Adhabu*

Makadirio ya riba na adhabu

**81.**-(1) Kamishna Mkuu atafanya makadirio ya riba na adhabu ambazo mtu anatakiwa kulipa chini ya Sehemu hii.

(2) Deni la riba na adhabu iliyotolewa chini ya Sehemu hii kuhusiana na kutokutenda au maelezo yatahesabiwa kwa kutumika kwa kila kifungu cha Sehemu hii.

(3) Riba na adhabu inayotozwa chini ya sehemu hii ni pamoja na kodi nyingine yoyote iliyotozwa kodi na sheria ya kodi na haimuondolei mtu yoyote wajibu wa kushtakiwa kwa shauri la jinai.

(4) Iwapo kutokufanyika kwa jambo au kutokutolewa kwa maelezo kunasababisha kutozwa kwa riba au adhabu chini ya sheria hii na sheria nyingine ya kodi, Kamishna Mkuu atakadiria riba kwa mtu huyo chini ya sheria mojawapo pekee inayotoa kiwango cha juu cha riba au adhabu.

(5) Endapo makadirio yatafanyika chini ya kifungu hiki, Kamishna Mkuu atatakiwa kutoa taarifa ya makadirio ambayo yanaweza kujumuishwa kwenye taarifa nyingine ya makadirio iliyotolewa kwa mtu huyo chini ya sheria ya kodi, ikielezea-

- (a) jina la mtu na Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi;
- (b) kiasi cha riba au adhabu kama kilivyokadiriwa na Kamishna Mkuu;
- (c) namna makadirio yalivyokokotolewa;
- (d) sababu zilizosababisha Kamishna Mkuu kufanya makadirio;
- (e) tarehe ambayo riba au adhabu zitatakiwa kulipwa; na
- (f) muda, mahali na namna ya kupinga makadirio.

(6) Makadirio yanayofanywa chini ya kifungu hiki yatatambulika kama makadirio halisi kwa madhumuni ya kifungu cha 48.



*(d) Makosa*

Kosa la  
kushindwa  
kutekeleza  
matakwa ya  
sheria ya kodi

**82.** Mtu anayeshindwa kutekeleza mashrti ya sheria hii anatenda kosa na atawajibika iwapo atatiwa hatiani atawajibika-

- (a) ikiwa kutokutekeleza huko kutasababisha au, kama kusingegundulika, malipo ya chini ya kodi kwa kiasi kisichozidi pointi 50 ya thamani halisi ya fedha atalipa kiasi kisichopungua pointi 20 ya thamani halisi ya fedha na si zaidi ya pointi 50 ya thamani halisi ya fedha au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au vyote pamoja; na
- (b) ikiwa katika hali nyingine yoyote, kulipa faini isiyopungua pointi 10 ya thamani halisi isiyozidi pointi 20 ya thamani halisi ya fedha.

Kosa la  
kushindwa  
kulipa kodi

**83.** Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa kodi yoyote ndani ya au kabla ya tarehe ambayo kodi hiyo ilitakiwa kulipwa, anatenda kosa na iwapo atatiwa hatiani, atawajibika-

- (a) iwapo anashindwa kulipa kiasi cha ziada cha pointi 50 ya thamani halisi atalipa kiasi kisichopungua pointi 25 na si zaidi ya pointi 100 au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja; au
- (b) katika hali nyingine yoyote, kulipa faini isiyopungua pointi 10 ya thamani halisi ya fedha na si zaidi ya pointi 25 ya thamani

halisi ya fedha au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja na kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Kosa la kufanya au kutumia nyaraka au taarifa ya uongo au ya kupotosha

**84.**-(1) Mtu yeyote ambaye, katika jambo lolote linalohusu ushuru-

- (a) akiingiza kwenye jengo, chumba chumba, sehemu au mmea wowote, ambacho ni cha uongo au kimekosewa; au
- (b) anatoa au anasababisha tamko lolote, hati, maombi, marejesho, taarifa, au nyaraka nyingine yoyote ambayo ni ya uongo; au
- (c) iwapo atahitajika kujibu swali lolote lililoulizwa na ofisa wa kodi, na anakataa kujibu swali hilo au anatoa maelezo ya uongo au yasiyo sahihi wakati wa kujibu swali; au
- (d) kwa namna yoyote ile huku akiwa anajua anajihusisha na kukwepa kulipa kodi kwa njia ya udanganyifu; au
- (e) anajipatia msamaha, fidia au marejesho ya kodi ambayo kwa ufahamu wake hakustahili kupata;
- (f) anatoa maelezo ya uongo, anajitambulisha kwa udanganyifu kwa lengo la kupata msamaha, fidia au marejesho ya kodi;
- (g) anachukua, anatumza, anaficha, anaondoa au kwa namna yoyote ile, anajishughulisha na

bidhaa zinazotozwa ushuru ambazo zimetengenezwa au ambazo hazijalipiwa ushuru wa bidhaa; au

- (h) anaghushi, au kwa namna yoyote ile anatengeneza nyaraka bandia au akiwa anajua anatumia kitu kilichoghushiwa au kilicho bandia au anatumia nyaraka inayotakiwa au iliyotolewa kwa madhumuni ya ushuru wa bidhaa,

atatenda kosa.

(2) Mtu yeyote ambaye katika jambo lolote linalohusu sheria ya kodi-

- (a) anatoa tamko kwa afisa wa kodi ambalo ni la uongo au la kupotosha kwa namna yoyote ile; au

- (b) anashindwa kujumuisha katika tamko alilolitoa kwa afisa wa kodi jambo lolote ambao kutojumuishwa kwenye tamko kunalifanya tamko hilo kuwa batili kwa wakati huo, atakuwa ametenda kosa.

(3) Mtu aliyetenda kosa chini ya kifungo hiki, iwapo atapatikana na hatia, atawajibika-

- (a) iwapo maelezo au hali ya kutokutenda kulifanyika bila sababu ya msingi-

- (i) na iwapo dosari katika maelezo haikugundulika na kusababisha kufanyika kwa malipo pungufu ya kodi kwa kiwango kinachozidi pointi 50 ya thamani halisi ya fedha, atalipa faini isiyopungua pointi 25 ya thamani halisi ya fedha na si zaidi ya pointi 100 au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja; na

- (ii) katika hali nyingine yeyote, kulipa faini isiyopungua pointi 10 ya thamani halisi ya fedha na isiyopungua pointi 25 ya

thamani halisi ya fedha au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja na kisichozidi miezi mitatu au vyote; au

(b) iwapo maelezo au hali ya kutokutenda kunafanyika kwa maksudi au kwa uzembe -

(i) na iwapo dosari kwenye maelezo inagundulika, na inaweza kuwa imepelekea kulipwa kwa malipo pungufu ya kodi kwa kiwango kisichozidi pointi 50 ya thamani halisi ya fedha, kulipa faini isiyopungua pointi 50 ya thamani halisi ya fedha na isiyozidi pointi 200 ya thamani halisi ya fedha au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au vyote; na

(ii) katika hali nyingine yoyote, kulipa faini isiyopungua pointi 20 ya thamani halisi ya fedha na isiyozidi ya pointi 50 thamani halisi ya fedha au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au vyote.

(4) Kwa madhumuni ya kuamua iwapo maelezo yatatolewa kwa Kamishna Mkuu au la au ni lini maelezo hayo yatachukuliwa kuwa ni ya uongo au inapotosha, masharti ya kifungu cha 79 (4) na (5) yatatumika.

Kosa la  
kumzuia  
msimamizi wa  
kodi

**85.-**(1) Mtu anayezuia au anayejaribu kuzuia utekelezaji wa sheria ya kodi atatenda kosa.

(2) Mtu anayetenda kosa chini ya kifungu hiki, iwapo atatiwa hatiani, atawajibika-

- (a) iwapo kosa linahusu udanganyifu au ulaghai, kulipa faini ya mara mbili ya kiasi kilichokwepwa au kilicholipwa pointi 200 ya thamani halisi ya fedha 200, chochote kilicho kikubwa zaidi au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka minne au vyote.
- (b) iwapo ni katika hali nyingine yoyote, kulipa faini isipungua pointi 10 ya thamani ya halisi ya fedha na isiyo zaidi pointi 200 ya thamani halisi ya fedha au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au vyote.
- (3) Katika kifungu hiki, “kuzuia usimamizi wa sheria ya kodi” inajumisha-
  - (a) iwapo afisa wa kodi anatekeleza majukumu yake chini ya sheria ya kodi, kushambulia, kuzuia au kujaribu kushambulia au kumzuia afisa huyo au kuingilia mali yoyote inayotumiwa na afisa huyo;
